



DELIVERED FROM THE POWERS OF DARKNESS

By Emmanuel ENI

"For we are not fighting against people made of flesh and blood, but against the evil rulers and authorities of the unseen world, against those mighty powers of darkness who rule this world, and against wicked spirits in the heavenly realms." Ephesians 6:12.

KUKOMBOLEWA KUTOKA KWENYE NGUVU ZA GIZA

na Emmanuel ENI

www.DivineRevelations.info/SWAHILI

Sura 1: Nilipotorokea kwenye "Maisha mapya"

"Mfunze mtoto namna ya kuishi vizuri, naye hatasahau njia hiyo hata uzeeni." (Mithali 22: 6).

Hii ni simulizi ya Kazi ya Mungu- yenyne nguvu, ya ajabu naya kushangaza- katika kutii amri ya YESU KRISTO akiniambia: *"Nenda na ushuhudie kile nilichokufanyia"*

Mara nyingi mtu anadhani bahati mbaya ni kama kitendo cha kukosa na kwamba hatuwezi kufanya chochote kubadilisha matokeo ya maisha yetu. Kwa kiasi fulani hii ni kweli. Katika kesi ya mtoto wa Mungu, maisha yake yamepangwa (Mithali 16: 9). Hata kama mpango huo umetimia au bado inategemea na sababu mbalimbali, ukaribu wa mtu binafsi na Mungu, mtazamo wake kuhusu madhumuni ya mwisho ya maisha, na mazingira ya kijamii na kiroho anayojikuta akiwa mwenyewe ndani yake.

Safari ya maisha yako inakuwa na changamoto kwa sababu baadhi za nje. Tabu inakuja pale unapotoa Uhuru wako kwa njia moja au nyingine, kwa wema au ubaya. Unaweza kupenda au ukachukia. Unaweza taka kuelewa au kutoelewa . Utayari wa kutii ni nguvu kubwa ya Mkristo mpya aliyezaliwa, wakati utayari wa kuasi ni nguvu kubwa ya kuharibu kwa mtenda dhambi.

Mtoto anapoachwa peke yake katika dunia anatawaliwa na moja ya mamlaka hizi mbili: nzuri au mbaya, sahihi au isiyo sahihi , Mungu au shetani. Kila mtu anapimwa na nguvu hizi mbili za maisha, na kila mmoja ni lazima achague maisha yapi ni lazima aishi. Na naamini kwamba hivyo ndivyo Biblia inasema: "Mfunze mtoto namna ya kuishi vizuri, naye hatasahau njia hiyo hata uzeeni.". Utakubaliana nami kuwa mtu wa karibu sana na kipenzi cha moyo wa mtoto ye yeyote ni mama yake.Yatima ni mtoto mwenye bahati mbaya na wazi kuwa ameachiliwa katika mashambulizi ya shetani zaidi kuliko watoto wenyewe wazazi . Mama ni mlinzi wa mwili na roho lakini inakuwa ni janga mara mbili pale wazazi wote wawili wamepotea na zaidi sana katika mazingira ya utata. Hadithi yangu inaanza miaka 22 iliyopita katika kijiji kidogo kinachoitwa Amerie Iriegbu Ozu Item katika Ma mlaka ya Serikali za Mitaa Bende, jimbo la Imo. Wazazi wangu walikuwa si katika kundi la mionganoni mwa tajiri lakini baba yangu alikuwa na neema ya kurithi hekta 42 za ardhi kutoka kwa babu yangu , baraka ambayo leo hii imenisababishia bahati mbaya sana ambayo haikuwahi kutokea katika historia ya familia. Baba yangu alichukiwa sana na ndugu zake wa mbali na karibu kwa sababu ambazo mimi sizijui, labda kwa sababu ya urithi wake mkubwa wa ardhi.

Tulikuwa ni familia yenyne furaha, wazazi wangu baada ya kutupata sisi wanne: Love , Margaret , Emmanuel na Chinyere . Baada ya kuwa na mabinti wawili wa kwanza , wazazi wangu walisubiri kwa miaka 14 kabla ya kunipata mimi (mwana pekee wa kiume) na baadaye dada yangu mdogo Chinyere . Hii ililetu furaha ya kweli kwa familia, lakini furaha hii ilikuwa ni ya muda mfupi tu baada ya janga la kwanza kutokea . Mama yangu mpenzi na anayejali alikuwa. Ilidaiwa kuwa alikuwa kutohana na uchawi, na miaka minne baadaye baba yangu alifariki, tena ilidaiwa kuwa naye ni kwa njia ya juju iliyofanywa dhidi yake. Miaka miwili baada ya kifo cha wazazi wote wawili, dada yangu mkubwa,Love, alitoweka kimaajabu na Margaret, binti wa pili wa wazazi wangu akachanganyikiwa akili. Ilikuwa ni molongo wa majanga katika maisha ya familia yenyne unyenyekevu na furaha. Dada yangu mdogo Chinyere na mimi tulipelekwa kwa babu na bibi yetu. Pale nilimaliza elimu yangu ya msingi na baadaye nilijiunga na Item High School. Nilisoma mpaka darasa la III la shule ya sekondari na nikaacha kwa sababu ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya ada n.k. Muda mfupi baada ya hili, babu na bibi pia walikufa. Baada ya

sherehe zote za mazishi, ndugu yangu nisiyemjua alimchukua dada yangu mdo Chinyere , na hadi leo hii sijui yuko wapi. Kwa sababu ya malezi mabaya, nililazimika kurudi kwenye nyumba ya baba yangu, na kuishi huko peke yangu katika umri wa miaka 13. Jinsi gani mtoto wa miaka 13 anajilisha mwenyewe katikati ya maadui wa baba yake na yeye mwenyewe? Jinsi gani nilivyokuwa Naogopa! Matuukio haya yalioneckana kama yamenileta katika mwisho wa kuishi. Je kulikuwa na mtu aliyejali? Je kuna yeote aliyehusika na "**Mikosi ya kijana huyo mdo**?"

Siku moja nilikutana na rafiki niliyemjua nilopokuwa shule ya msingi aitwaye Chinedum Onwukwe . Chinedum alinipenda sana na waliposikia yote yaliyonisibu alinichukua mpaka kwa wazazi wake ambao kwa urahisi tu walnipokea na kunifanya kama mwana wao wa pili. Maisha yakaja tena kawaida.Walinijali vyema. Nilikuwa na furaha tena: Sasa nilijua kuwa Mungu wa mama yangu aliyuombwa wakati aliokuwa hai alikuwa hai mahali fulani hivi. Amenipatia wazazi wapya, ndivyo nilivyojiwazia, nilfurahia wema huu kwa miaka miwili na kisha shetani akapiga tena .

Chinedum na wazazi wake walikuwa wakisafiri kuelekea Umuahia na gari yao ikaingia ndani ya tipa lilolobea mzigo kama udongo. Chinedum na wazazi wake walikufa papo hapo! Baada ya kusikia habari hizi niliduwaa. Huzuni yangu inaweza tu kufikirika. Niliweza kuvumilia kipindi chote cha sherehe za mazishi, Nikiwatafutia wale wapishi kuni za kupikia na shughuli zingine: na mwishoni mwa hayo nikarudi nyumbani kwa baba yangu na nikarudia tena ajira hafifu ili niwe na uwezo wa kujilisha.

Niliendelea kufanya kazi zisizo za kawaida katika mashamba, katika bustani, kuvua samaki pamoja na wazee mpaka siku moja, mtu mmoja katika eneo langu alinikodisha kufanya kazi katika shamba lake kwa 50k . Pale shambani alinikabili kwa mlolongo wa maswali. Kwanza, akanionba nimuonyeshe ardhi ya baba yangu, pili, nimkabidhi shamba hilo, bila kujali jinsi uhusiano wetu ulivyokuwa. Katika kesi zote hizo mimi nilipinga na alikasirika. Kisha aliapa kuniua katika msitu. Nikawa na hofu nikakimbia na kupiga kelele ili nipate msaada. Kwa bahati mbaya, kwa sababu eneo hilo lilikuwa mbali na ni ndani ya msitu mnene hakuna mtu aliyesimama kwa msaada lakini msaada ultoka kwa Mungu.

Alinikimbiza na kisu chake lakini kwa kuwa nilikuwa mdo nilikimbia haraka sana kuliko yeye nilianguka ndani ya shimo lenye kina cha mita 1.82 hivi na nilifunikwa na majani yaliyokua ndani yake. Naye akatafuta na baada ya muda akakata tamaa . Baadaye nilijitahidi kutoka nje ya shimo na kupitia njia nyingine nikarudi kijijini.Nilitoa taarifa ya tukio hilo kwa wazee wa eneo letu lakini hakuna hatua zilizochukuliwa - kawaida ya watoto yatima. Tukio hili liliunda chuki kubwa katika moyo wangu mdo, hakuna mtu alinipenda, hakuna aliyenifikiria na kunijali.

Nilitafakari kwenye mawazo yangu kwa nini mtu yeote alitaka kuniua baada ya kujua kuwa mimi sikuwa na wazazi . Maisha yalijawa na taabu. Sasa najua ya kuwa Mungu katika upendo wake alimzuia shetani asinichochee wazo la kwenda kujiua. Nilimgeukia Mungu na kuwa mwanachama kamili wa Kanisa la Assemblies of God katika kijiji changu (bado nipo) lakini kwa bahati mbaya hakuna aliyejali ingawa hata baadhi ya wapendwa walijua kwa habari yangu. Ni muhimu kutambua kwamba nilikuwa mwanachama kamili wa kanisa bila kumjua Yesu Kristo. Sikujua nini maana ya kuzaliwa mara ya pili . Kama wewe uko katika Kanisa la Yesu Kristo na unajikuta katika hali ambayo nilijikuta, mkabidhi Bwana Yesu Kristo maisha yako. Maandiko yanasema: "*7Mwekeeni matatizo yenu yote, maana yeye anawatunzeni.*" (1 Peter5 : 7).

Katikati ya ugumu huu wa maisha na mateso ALICE alitokea! Alice alikuwa msichana niliyemjua wakati wa siku zangu za shule ya msingi. Alikuwa na miaka mitano zaidi yangu tulitokea kijiji kimoja. Tulikuwa darasa moja,tuliketi kwenye benchi moja na akawa rafiki yangu sana. Na 'upendo' huu katika hali ya utoto, tuliweka ahadi ya ' kufunga ndoa ' wakati tukiwa wakubwa. **Mzaha!** Mtoto wa miaka 11 wakati huo, bila wazazi, sina elimu , sina chakula , naweka ahadi ya ndoa kwa msichana wa miaka mitano zaidi yangu! Alice baadaye aliondoka

na kwenda Akure kwa elimu yake ya sekondari na alinitumia barua za 'upendo' nyingi.

Wakati mwingine nilipokutana na Alice , nilikuwa nina miaka 15 na yeye alikuwa 20. Yeye alipomaliza elimu yake ya sekondari alifanya kazi na Benki ya Standard Lagos (sasa Benki ya Kwanza), ambapo wazazi wake walikuwa wakiishi.

Alice akiwa anajua historia yangu na matatizo yangu aliichukua hii kama fursa. Aliniambia nijiunge naye Lagos na akanipa anuani yake pamoja na N50 (naira : Sarafu ya Taifa ya Nigeria)! Hiyo ilikuwa ni bahati kwa kijana wa miaka 15 ambaye hakuwahi kupata N2 kwa siku! Hii ilikuwa ni mana kutoka mbinguni na hii ilimaanisha kuwa Lagos lazima palikuwa ni mahali pa ajabu penye fedha nyingi na mambo mema ya maisha kwa wote kufurahia. Ni lazima kwenda Lagos kutengeneza pesa yangu mwenyewe na kupata utajiri pia . Kwenda Lagos kwa akili yangu ilikuwa ni njia pekee ya kutoroka. Kukimbia kutoka kwa maadui wa baba yangu, kukimbia kutoka kwa madui zangu, kutoroka kutoka kwenye njaa na matatizo yangu yote. Kukimbia! Kukimbia! Ndiyo, kukimbia kutoka katika yote yale ambayo ni mabaya!!!

Sura 2: Mwanzo

« Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti. » Mithali 14:12

« Bali wabaya wanafanana na bahari iliyochafuka; maana haiwezi kutulia, na maji yake hutoa tope na takataka. Hapana amani kwa wabaya; asema Mungu wangu. » Isaya 57: 20-21

Na maisha ya nje ya Yesu Kristo ni sawa na ilivyoelezwa katika maandiko hapo juu. Niliondoka katika kijiji changu na N50 na anwani niliyopewa na Alice, kukimbilia **uhuru, haki, starehe** na yote yanayokwenda pamoja nayo: lakini kama utakavyoona hapo baadaye ilikuwa ni tofauti sana na kile nilichofikiria kwenye moyo wangu mdogo. Nilipofika Lagos , ilikuwa ni nzuri sana katika macho yangu na niliilinganisha na Mbinguni, chochote kile Mbinguni kulivyofanana. Niliona yale majengo yote marefu na mazuri na katika kila uso niliweza kuona furaha (hivyo nikajiwazia). Watu walionekana kuwa na shughuli nyingi sana na kila mmoja alijali mambo/ biashara yake. Nilipatwa na msisimko na nikajisemea moyoni , "**Sasa nimejua kuwa niko Huru!**

Niliwasili Akintola Road, Victoria Island na nilipokelewa vizuri na Alice na wazazi wake. Wazazi wake walini jua mimi na historia yangu kwa sababu tunatoka katika kijiji kimoja lakini kamwe hawaku jua uhusiano wangu na binti yao. Alice alinitambulisha tena kama kijana aliyemchagua amuo. Wazazi walish tuka lakini baada ya majadiliano naye, walikubaliana juu ya hali yangu kwamba wangeweza kuniende leza kielimu kwanza. Alice alikataa pendekezo lao na akaomba niwe ninaishi naye katika gorofa yake mwenyewe. Wazazi hawaku weza kukubaliana na hili lakini alisisitiza. Walikuwa na mabishano kuhusu hili kwa siku nne na kwa ushawishi usioelezeka walikubali na nikaishi na Alice.

Alice, msichana ambaye ni mzuri sana, aliniambia kuwa alikuwa ni mhasibu wa Benki ya Standard na kwamba angeweza kunifanya mimi tajiri na kunipa vyote navyovihitaji katika maisha haya na alisema: " wewe kaa tu na ufurahie!" Mtazamo wangu ya kwanza kuhusu Lagos kumbe ulikuwa ni kweli; miezi michache iliyopita nilikuwa katika kibanda kidogo katika kijiji kidogo kulichozungukwa na chuki, njaa na mateso na mimi hapa, tazama ninaishi katika mji mkubwa, ghorofa nzuri na ' mke ' mzuri ambaye aliniahidi kunipa maisha ye yote kadiri yanavyotoa. Alinimwagia zawadi, fedha , mavazi, 'upendo' nk Mimi siku wahai kamwe kujua kwamba dunia ime jaa haya ' mambo mema . Shetani kweli ni mdanganyifu ! Maandiko dhahiri yanasema : " Mwizi haji isipokuwa kuiba, kuua na kuharibu. Mwana pekee wa adamu (Yesu Kristo) anayeweza kukupa uhai na kukupa zaidi "(Yohana 10: 10). Ndugu msomaji, shetani hana zawadi ya bure ! Chochote anachokupa ni kwa ajili ya kui pata roho yako . Hali hii ya furaha ilikuwa ya muda mfupi, kwa sababu baada ya muda wa miezi mitatu mambo ya ajabu yalianza kutokeea.

Uzoefu wa Kushangaza

Usiku mmoja, niliamka usiku wa manane na nikaona nyoka mkubwa aina ya boa - constrictor kando yangu. Nilitaka kupiga kelele lakini sikuweza. Usiku mwingine, niliamka na kuona mwili wa Alice kama unaoangaza kama mifuko ya Cellophane. Usiku mwingine, alitoweka na kutokeea tena na tena. Usiku mwingine nilisikia kelele za ajabu au kuchenza katika sebule n.k. Sikuweza kuvumilia tena matukio haya ya kutisha hivyo niliamua kumuliza, na jibu la kwanza ilikuwa ni vurugu na onyo kali. Alisema: " Usiniulize swali hili tena au nitapambana na wewe. "

Tangu wakati huo nilijua maisha yangu yalikuwa hatarini. Niliona ni afadhali mateso kijijini kuliko kile nilichokuja kugundua. Nikawa ninamhofia. Siku mbili zikapita na akaja na tabasamu, zawadi na akanikumbatia. Akaniambia jinsi gani anavyonipenda na kunijali na akaniambia nisiwe na hofu na aliahidi kunieleza mambo

fulani hapo baadaye. Alinichukua mpaka klabu na usiku ule alinikumbusha ahadi yake ya kunifanya mimi tajiri nk, na aliniambia: "Siku moja utajua yote ninayoyafahamu ! " Tukarudi nyumbani na maisha yakaendelea kama kawaida kati yetu. Ndani nilijua nilikuwa katika hatari , lakini nitawezaje kutoroka na wapi nitatorokea? Ni muhimu kukumbuka hapa kwamba wazazi wa Alice hawakumjua binti yao, ingawa ni mdogo, alijihuisha sana na uchawi na mizimu na alinionya sana kamwe nisije kuwaambia kama ninayapenda maisha yangu. Ndugu msomaji, unaweza kufikiria , msichana mwenye umri wa miaka 20 anafanya mambo haya yote? Dunia ya nje ilimwona kama msichana mzuri sana na mpole anayefanya kazi na Benki kubwa lakini alikuwa ni wakala mkubwa wa shetani. Kuna akina Alice wengi katika dunia ya leo kama utakavyokuta baadaye katika kitabu hiki.

Ugunduzi wa Kutisha

Siku moja, baada ya yeze kuondoka kwenda kazini, niliamua kufanya ukaguzi katika ghorofa. Pamoja na ujana aliokuwa nao, gorofa ilikuwa imejazwa vya kutosha. Alikuwa na friji nne na baada ya kufungua friji moja, niliona fuvu la binadamu, sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu safi na kavu. Ndani ya dari kulikuwa na mifupa. Katika kona nyingine moja ya vyumba nikaona (kile baadaye nilijua kama 'chamber') sufuria imejaa damu na mti mdogo katikati ya sufuria, kibuyu na nguo nyekundu pamoja nacho. Sikuweza kuendelea. Sasa nilijua kwamba nilikuwa ni mtu mfu na kwa kuwa sikuwa na mahali pa kukimbilia. niliyatoa maisha yangu kwa chochote kitakachokuja, maisha au kifo na naliendelea kufunga mdomo. Alice akarudi kutoka kazini na nilijua kabisa katika ofisi yake kuwa alijua nini nilichokifanya katika nyumba.

Kuingia katika ulimwengu wa Kichawi

Siku iliyofuata aliniomba nimfuate kwenye mkutano. Nilikuwa tayari ni mfungwa na sikuwa na uchaguzi. Tulikwenda kwenye jengo kubwa sana nje kidogo ya Lagos. Tulipowasili (jengo lilikuwa na ukumbi wa mkutano chini ya ardhi), nilielekezwa na Alice kuingia kinyumanyuma. Nilimtii na niliingia kwa mgongo, yeze pia alifanya hivyo. Ukumbi ulikuwa mkubwa wenyewe vijana na wanawake500 wameketi katika mduara, na aliyekuwa ameleti juu yao alikuwa ni mtu ambaye kichwa chake ndicho kiliweza kuonekana lakini hakikuwa na mwili, kama Kiongozi. Baadhi ya vijana hawa walikuwa wanafunzi, wanafunzi wa vyuo vikuu, wahitimu, walimu nk Alice akabonyeza kiswichi ukutani na kiti kikakatoka chini ya ardhi nami nikaketi. Yeze naye alifanya hivyo na kiti kingine kikatoka kwa ajili yake naye akaketi. Akanitambulisha katika mkutano ule kama mwanachama mpya na wao wakampongeza na kunikaribisha. Alice alikuzwa nafasi kwa sababu ya hili. Yote waliyoyajadili katika mkutano mimi sikuyalewa. Mwishoni mwa kikao na tulipokuwa karibu kuondoka, niliambiwa nirudi peke yangu siku iliyofuata na Kiongozi. Hii ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kukutana na dunia ya uchawi.

Usiku huo huo, saa 2:00 (na hii ni saa ya kawaida ya mikutano na shughuli hatari za nguvu zote za giza na mawakala wao), Alice aliniamsa na akanifunulia mambo fulani. Alisema: "Mimi si binadamu wa kawaida. Mimi ni nusu binadamu na nusu roho lakini hasa ni wa rohoni. Unachokiona katika kona ya chumba changu ndicho natumia wakati wa maombi yangu ya kila asubuhi, ili roho zile ziniongoze kwa siku nzima. Kwa habari ya mifupa mimi nitakuambia baadaye. "

Sikusema neno. Alileta baadhi ya vitabu juu ya siri za dunia kwa ajili yangu kusoma, na kwa sababu ya shauku ya kutaka kujua niliamua kuvisoma. Muda mfupi tu nilivipenda na akaona kuwa nimevipenda.Bila ya mimi kujua alituma jina langu katika jamii ya kichawi huko India. Kama nilivyokuwa nimekwisha elekezwa, siku iliyofuata nilikwenda peke yangu kwenye ile jamii na nikakutana na wengine tisa na baadhi ya mashahidi. Ilikuwa tunaingizwa rasmi. Tuliitwa pale katikati ya ukumbi na mambo yafuatayo tulifanyiwa:

1. Mchanganyiko unaoonekana kama putty ulipitishwa juu ya miili yetu. Hii inakufanya uwe **mwanacham a kamili**.
2. Glass yenye kimiminika kama mafuta tulipewa kunywa. Hii inakufanya kuwa **wakala**.
3. Unga ulio kama wa risasi ulipakwa katika vichwa vyetu. Hii inakufanya uwe na uwezo wa kujifunza siri zao.

Bila kujua, hii sherehe kumbe ilikuwa ikirekodiwa India na Siku ya pili nilipokea barua kutoka kwao. Katika barua nilielekezwa nitie doa kwa damu yangu mwenyewe na baada ya hilo niitume tena kwao kwa njia waliyoielekeza, si ya Posta. Nilifanya. Kutokea siku hii hakuna kurudi nyuma; kurudi nyuma ina maana ni kifo kama mmoja wao mara zote walnikumbusha hili na nilijua kuwa hakukuwa na matumaini tena kwa ajili yangu.

Makataba na Alice

Asubuhi moja mapema, aliniambia kulikuwa na sherehe muhimu inayotakiwa kufanya katika nyumba. Saa 2:00 usiku alileta mtoto anayetambaa, msichana, hai. Mbele ya macho yangu, Alice alitumia vidole vyake kunyofoa macho ya mtoto. Kilio cha mtoto yule kiliuvunja moyo wangu. Kisha akamchinja na kumkata mtoto vipande vipande na akaweka damu na mwili ndani ya tray na akaniambia nile. Nilikataa. Aliniangalia moja kwa moja kwenye macho yangu na kile kilichotoka kwenye macho yake hakiwezi kuelezeza kwa maandishi. Kabla sijatahamaki nini kinatokea nilikuwa si tu natafuna nyama lakini pia nilikuwa nakunywa damu. Wakati haya yanatokea, alisema: "Hii ni mkataba kati yetu sisi, kamwe hutokuja kusema nje chochote una chokiona mimi nakifanya au chochote kuhusu mimi kwa binadamu ye yeyote duniani. Siku ukivunja ahadi hii basi utakuwa umeondoka. "ikiwa inamaanisha kuwa siku nikivunja mkataba huu nitauawa.

Baada ya tukio hili nilianza kuwa na hisia za ajabu ndani yangu. Nilibadilika na sikuweza kujizuia. Neno la onyo kwa akina mama. Je, unawajua wasaidizi wa nyumba yako? Ni viyi historia yake inafanana? Je, unajali kujua yote kuhusu yeye kabla ya kumkabidhi maisha ya watoto wako nk? Jinsi gani Alice alimpata mtoto anayetambaa na kumchinja, unaweza kujuliza. Kwa hiyo wazazi, unatakiwa kujua historia ya wasaidizi wenu.

Pale Alice alipoona kwamba amefanikiwa kunifanya kikamilifu kujihusisha na ulimwengu wa mapepo na nilikuwa nikiongezeka kwa kasi katika hilo, aliridhika na alijua mkakati wake umekamilika. Alinitafutia gorofa kwa ajili yangu, alinisaidia kuimalizia na baada ya hapo akajitenga na uhusiano.

Mkataba nchini India

Jumuiya ya Delhi, India ilinitumia barua ya pili ikinisihi niende India. Ndani ya barua pia walnielekeza nifanye yafuatayo: " Kula kinyesi, kula panya waliooza na wanaonuka, na kufanya ngono na mapepo katika makaburi wakati wa usiku"

Baada ya kutimiza hayo hapo juu nilifungwa nisifanye ngono na mwanamke ye yeyote duniani. Nilituma majibu india nikiwataarifu kuwa sikuwa na visa na sijui jinsi ya kufika india. Kwa wakati huu nilikuwa nimeanza kufanya 'biashara'. Nilikuwa ni mfanyabiashara kiharamu mkubwa lakini kwa sababu ya nguvu hizi nyuma yangu sikuwa na shida na watu wa bandari nk

Nilianza kuwa na fedha nyingi, chakula na vitu havikuwa tena adimu. Siku moja, nilifunga gorofa yangu na nikatoka; niliporudi, nikafungua mlango na tazama, mtu ameketi katika sebule. Niliogopa. Akasema: "Je, wewe

si Emmanuel Amos?" nikamjibu ni mimi. Akasema: " nimeatumwa kuja kukuchukua twende zetu India, Hivyo jitayarische." Nilifunga kila mahali, nikaenda na kuketi kandokando yake nikisubiri amri inayofuata. Lakini kama umeme, alinigusa na tukatoweka kabisa.

Sehemu iliyofuata nilijikuta niko mwenyewe ilikuwa ni kwenye ukumbi mkubwa wa mkutano Delhi, India, pamoja na umati wa watu wengine waliokuwa wamekaa tayari kwa ajili ya kutukaribisha. Walileta mafaili ambapo jina langu lilikuwa tayari limeandikwa na akaniambia niweke sahihi yangu pembeni.Nikafanya. Sahani iliyokuwa na nyama mbichi za watu, zilizokatwa vipande vipande na basini ya damu vililetwa. Jagi tupu za maji zililetwa na kila mtu akapewa yake,kasha mtu asiyekuwa na kichwa akawa akipita huku akimimina damu na nyama katika jagi zetu. Mishumaa tofauti tofauti iliwaka pamoja na ubani. Mwanaume asiyekuwa na kichwa akafanya manuizo na kila mtu akanywa damu na nyama na mkutano ukaisha.

Uingizwaji nchini India

Sasa kipindi cha kupimwa kikafika. Nilipelekwa kwenye bonde lenye mita 200 kwa urefu. Ndani yake kulikuwa na mchanganyiko wa nyoka hatari na wanyama pori . Sikutakiwa kupiga kelele kwa sababu kama nikipiga kelele bai nimeshindwa mtihani na adhabu yake ilikuwa ni KIFO. Baada ya siku saba za uchungu nililetwa kwenye sehemu ilioitwa ' INDIA JUNGLE'.

Katika msitu huu niliona aina tofauti za ndege wa kipepo; ni ndege wa kipepo kwa sababu sura za ndege hawa zingine zilikuwa ni za mbwa, baadhi kama paka, n.k lakini wakiwa na mabawa.Ndani ya Msitu kulikuwa na pango na pango hilo lilifunguliwa tu na hawa ndege mapepo. Walifungua pango na nikaingia ndani. Mambo niliyoona ni vigumu kuelezea. Kulikuwa na viumbe wa kutisha, baadhi walionekana kama binadamu lakini wana mikia na bila sura za watu, nk Hii ilikuwa ni sehemu nyingine ya mateso. Mateso yale yanaweza kuwa kama nusu ya kuzimu. Nilikuwa katika hali ile kwa siku 7 na kisha nilitolewa nje.

Kisha nilipelekwa kwenye maktaba kubwa sana yenye vitabu vikubwa na vya kipepo kwa ajili ya kujifunzia. Baadaye nilichukua vitabu viwili: Abyssinia , ambayo ina maana ya uharibifu, na Assina , ambayo ina maana kutoa uhai au kuponya. Baadaye nilipewa vitabu vingi zaidi. Nilipewa maelekezo ya kujenga chemba mara baada ya kurudi Nigeria na mambo yafuatayo ndani yake : " sufuria ya asili iliyojazwa damu ya binadamu, mti mbichi ndani yake, na fuvu la binadamu , manyoya ya tai , ngozi ya mnyama pori , ngozi ya nyoka na udongo unaon'gaa kando ya sufuria. " damu ndani ya chungu ilitakiwa kunywa kila asubuhi na dua. Nilipewa maelekezo kuwa nisije kula chakula kilichopikwa na binadamu na kwamba nitalishwa kimiujiza. Nilirudi Nigeria kwa njia hiyo hiyo niliyoienda, na kutekeleza yote .

Niliporudi nyumbani Nigeria

Sasa nilikuwa ni mmojawapo katika sehemu ya ulimwengu wa roho na ningeweza kusafiri popote pale sehemu yoyote duniani. Kwa mujibu wa vitabu nilivyoleta, ni kwamba viumbe wa kiroho (kipepo) wanaishi katika anga. Nilifikiri labda sasa wangeweza kuongeza nguvu yangu, hivyo niliamua kujaribu. Nilitoka nje ya nyumba yangu, nikafanya baadhi ya manuizo na kuita upopo wa kisulisuli nikatoweka. Nikajikuta mwenyewe katika anga na kuona hawa viumbe wa kipepo. Je, unataka nini waliniuliza; niliwaambia nataka nguvu.

Nilikuja tena duniani baada ya wiki mbili baada ya kupokea nguvu kutoka kwao. Kama nilivyosema hapo awali, Sikuweza kujizuia/kujidhibiti mwenyewe. Pamoja na nguvu zote hizi nilizokuwa tayari nimezipokea, bado nilihitaji nguvu zaidi na zaidi ! Hivyo niliamua kwenda chini ya ardhi ili kuthibitisha kile kilichoandikwa katika vitabu nilivyopewa.

Siku moja nilikwenda mahali fulani kichakani, nikafanya baadhi ya manuizo kama ilivyoelezwa kwenye vitabu nikaamuru ardhi kufunguka. Ardhi ikafunguka na mapepo yakaunda ngazi mara moja. Nikapiga hatua na kuingia moja kwa moja ndani ya ardhi. Kulikuwa na giza kuu ambalo linaweza tu kulinganishwa na moja ya mapigo ambayo yalitokea kule Misri kama iliyoandikwa katika Biblia. Niliona mambo mengi ambayo ni vigumu kueleza. Niliona watu walio katika minyororo, watu wanaotumika kwa ajili ya kutengeneza fedha - majukumu yao ilikuwa ni kufanya kazi mchana na usiku kukusanya fedha kwa watekaji wao.

Nikaona baadhi ya wanachama wasomi/wenye akili wa jamii ambao walifika kutoa baadhi ya sadaka na walirudi duniani na baadhi ya zawadi walizopewa na mapepo yanayotawala sehemu zile. Niliona baadhi ya viongozi wa makanisa ambao walikuja kwa ajili ya kupata nguvu, nguvu ya kusema jambo lolote na linakubaliwa bila ya kuhoji katika kanisa. Nilikaa kwa muda wa wiki mbili na kurudi baada ya kupokea nguvu zaidi. Watu waliniona kama mdogo nisie na hatia lakini hawakujua nilikuwa ni hatari. Kuna watu wengi kama hao katikati yetu; ni wale tu walio katika Kristo Yesu pekee ndiyo wako salama katika hali halisi ya usalama.

Mkataba na Malkia wa Pwani(Queen of The Coast)

Jioni moja, niliamua kutembea tembea. Barabara ya kituo cha mabasi cha Ebute Metta, nilimuona msichana/binti mrembo/mzuri amesimama. Sikuzungumza neno lolote. Siku ya pili nilipopita pia nikaona bado yuko pale pale. Siku ya tatu nikamuona tena bado amesimama pale pale na nikajitambulisha kwake kama Emmanuel Amos. Lakini yeeye alikataa kujitambulisha.

Mimi nikamuuliza jina lake na anwani lakini yeeye alicheka tu. Yeye akaniuliza yangu nami nilimuambia mtaani tu. Nilipokuwa nataka kuondoka, akasema atanitembelea siku moja. Kwenye mawazo yangu mimi nikasema, haiwezekani, sikumpa namba ya nyumba yangu basi sasa atawezaje kufika. Lakini ni kweli kwa maneno yake, nilisikia mlango wangu ukibisha baada ya wiki toka tumekutana pale katika kituo cha basi. Alikuwa ni yeeye, msichana wa ajabu! Nilimkaribisha lakini katika mawazo yangu (Nilijiuliza msichana huyu mzuri atakuwa ni nani, je, hajui kuwa alikuwa amekanya katika uwanja hatari?) Nilimfurahisha naye akaondoka. Baada ya ziara hii ya kwanza, ziara zake zikawa mara kwa mara bila uhusiano wowote.

Katika ziara zake alikuja kwa muda ule ule, na hakuja dakika moja kabla au iliyofuata! baadhi ya ziara zake nilipenda kumpeleka Lagos Barbeach, au katika Hoteli ya Paramount au Hoteli ya Ambassador nk Wakati wote huu, bado hakuniambia jina lake. Niliamua kutokuwa na wasiwasi kwani nilijua uhusiano wetu usingeendelea zaidi ya hapo. Nilikuwa nimepewa maelekezo kamwe nisiguse mwanamke.

Ghafla ziara zake zikawa ni usiku. Katika ziara yake moja aliniambia: "Sasa ni wakati wako wewe kunitembelea mimi." Tulikaa pamoja usiku na saa 2:00 asubuhi kesho yake tukachukuana. Tuliingia pamoja katika basi na alimwambia dereva atuache barbeach. Tuliposimama, nilimuuliza: "tunakwenda wapi?" Alisema: "Usijali, Utakwenda kufahamu nyumba yangu" alinipeleka kwenye kona ya barbeach, akatumia kitu kama mkanda na kuufunga ukituzunguka na mara moja nguvu fulani ikaja kutoka nyuma yetu na kutusukuma ndani ya bahari. Tukanza kupaa juu ya uso wa maji na moja kwa moja tukaingia ndani ya bahari. Ndugu msomaji, hiki kilitokea nikiwa katika mwili wangu! Wakati ule tumezama ndani chini kwenye kitako cha bahari kwa mshangao nikajiona tuko tunatembea kwenye barabara ya magari ya mwendo kasi . Tukaenda mpaka kwenye jiji lenye watu wengi na walio na shughuli sana.

Ulimwengu wa Roho

Niliona maabara nyingi, kama za maabara za sayansi, maabara za kubuni, na ukumbi wa michezo(theatre). Nyuma ya mji, niliona wasichana wazuri na vijana wazuri. Hakuna wazee. Akanitambulisha kwao na walinikaribisha. Akanipeleka kwenye sehemu kama "chumba cha giza", "chumba cha kukaushia", na "chumba cha kufungashia."

Akanipeleka mpaka kwenye kiwanda kikubwa na ghala kubwa na kisha akanileta kwenye nyumba yake binafsi. Pale alikaa kuniambia: "Mimi ni Malkia wa pwani (queen of the coast) na ningependa sana kufanya kazi na wewe. Nina kuhahidi nitakupa utajiri na vyote vinavyokwenda pamoja nayo, ulinzi na vyote vinavyokwenda na hayo, uzima na 'malaika' atakayekuongoza wewe."

Akabonyeza kidude na mwili wa binadamu mbichi ukaja (katika vipande) ndani ya trei(sahani) na tukala pamoja. Akaamuru boa (nyoka) aje na akaniambia nimmeze.sikuweza. Alisisitiza lakini sikuweza, ninawezaje kumeza nyoka aliyehai tena aina ya boa. Akutumia nguvu yake na nikammeza. Haya yalikuwa ni maagano matatu: **mwili wa binadamu na damu, boa(nyoka) na malaika mapepo** walikuwa pale siku zote ili kuhakikisha hakuna siri iliyowekwa wazi.

Lakini 'pepo' alipewa uwezo wa kuniadhibu kama nikienda tofauti na pia kiniletea chakula kutoka baharini wakati wowote nikiwa hapa duniani. Niliahidi kumtii siku zote daima. Na baada ya ahadi hii alinipeleka na sehemu nyingine ya bahari, Hii sasa ilikuwa ni kisiwa. Kulikuwa na miti na kila mmojawapo ya miti ulikuwa na kazi yake tofauti:

- Mti wa sumu,
- Mti wa mauaji,
- Mti wa kutaja/kuonyesha, na
- Mti kwa ajili ya tiba.

Alinipa nguvu ya kujibadili katika kila aina ya mnyama wa baharini kama kiboko, boa constrictor(Nyoka) na mamba na kisha akatoweka kabisa. Nilikaa katika bahari kwa wiki nzima kwa njia (kama ya mamba) aliyetajwa hapo juu nikarudi tena duniani.

Maabara za ulimwengu wa chini

Nilikaa Lagos kwa wiki moja nikarudi baharini, wakati huu nilikaa kwa miezi miwili. Nilikwenda katika maabara za kisayansi kuona nini kilichokuwa kinatokea. Nikaona madakitari wa akili na wanasayansi wanafanya kazi kwa umakini sana. Kazi ya wanasayansi hawa ni kubuni mambo mazuri kama magari ya kifahari, nk, silaha mpya na kujua siri za dunia hii. Na kama ingewezekana kujua nguzo ya dunia wanayoitaka, lakini Namshukuru Mungu, MUNGU TU ANAYEJUA.

Niliingia katika chumba cha kubuni na huko nikaona sampuli nyingi za nguo, manukato na aina mbalimbali za bidhaa za urembo. Mambo haya yote kulingana na Shetani ni kwa ajili ya kuvuruga mitazamo ya wanaume kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Niliona pia miundo/ubunifu tofauti ya umeme, kompyuta na kengele. Pia kulikuwa na TV ambapo walijua wale waliozaliwa tena kuwa Wakristo katika ulimwengu. Pale unawenza kuona na kutofautisha wale amba ni waendaji wa kanisani tu na wale amba ni Wakristo halisi.

Nikatoka katika maabara na kuingia katika 'chumba cha giza' na 'chumba cha kukaushia. Chumba cha giza ni mahali ambapo wanaua mwanachama yejote anayeasi. Wanamuua kwanza kwa kuchukua damu ya mtu huyo na kisha wanampeleka mtu huyo kwenye chumba chenye mashine ambapo itamsaga na kuwa unga kisha wanachukua unga na kuupeleka katika chumba cha kupakia ambapo wataufunga na kuupeleka kwa waganga wa kienyeji kwa ajili ya hirizi zao. Kulikuwa na mambo mengi ambayo ni vigumu kueleza kwa maandishi. Pamoja na nguvu yote hii ndani yangu, nilikuwa bado sijahitimu kukutana na Lucifer/shetani lakini tu nilikuwa na sifa ya kuwa wakala wake. Yote sawa,ila niliridhika kwamba mimi sasa nilikuwa na nguvu na ninaweza kukabili, changamoto na kuharibu vitu kadiri nipendavyo. Je, kunaweza kuwa na nguvu nyingine yoyote ile popote pale basi niliweka katika mawazo yangu.

Sura3: Utawala wa uovu

« *Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.* » Yohana 10:10

Nilipokuwa nikirudi Lagos, niliendelea na biashara yangu na baada ya wiki mbili nikarudi tena baharini. Malkia wa Pwani alinipa kile alichokiita "kazi yake ya kwanza". Nilitakiwa niende kijijini kwangu na kumuua mjomba wangu, mzee mmoja mganga maarufu aliyehusika kwa kifo cha wazazi wangu kulingana na taarifa yake huyo Malkia.

Nilimtii na nikaenda lakini kwa sababu sikuwahi kuua hapo mwanzo, sikuwa na ujasiri wa kumuua, badala yake nilimuhabibia dawa zake na kumuacha akiwa hana nguvu. Kwa sababu ya hili nililofanya alipoteza wateja wake wote mpaka leo hii. Nikarudi kutoa ripoti ya zoezi hilo lakini alikuwa hasira nami. Alisema matokeo ya kutokutii maelekezo yake ilikuwa ni kifo, lakini kwa sababu ya upendo wake kwangu atanituma tena nirudi kijijini na kuua wazee wawili ambaa alisema waliunga mkono suala la mauaji ya wazazi wangu. Kama hii ndio ilikuwa ni adhabu kwa kutotii maelekezo yake au sio, mimi sijui.

Hata hivyo, nilitii na nikarudi kijijini na 'niliweza' kuua watu hawa na kupeleka damu yao kwake. Kutokana na kitendo hiki kilichotokea katika mazingira ya kutatanisha ya kufa, wazee katika kijiji wakaenda kuuliza kwa mganga mwingine mwenye nguvu ambae kwa kawaida huwa anatuma radi kuchunguza muuaji ni nani. Kwa bahatimbaya kwa sabab ya watu hawa, nilikutana na mganga kiroho ambapo alikuwa akijaribu kuongea namapepo na nikamuonya asiseme chochote kama alipenda maisha yake. Alitoka nje na akawaambia wazee waende nyumbani na kuomba msamaha kwa mmoja kati ya watoto wao waliemuuzi na hakutaja jina langu.

Radi aliyoituma ikarudi na ikapiga katikati yao na kuua baadhi na kuacha wengi wamejeruhiwa. Baada ya tendo hili la kwanza, nguvu ndani yangu ilianza kujidhihirisha yenyewe. Nilimuumbua msichana yejote aliyekataa kufanya urafiki nami nk.

Mkutano wangu na Shetani

Nikarudi Lagos. Siku moja, msichana mmoja aliyeitwa NINA alikuja kwangu. NINA ambae wazazi wake wanatokea Jimbo la Anambra alikuwa mzuri na mrembo sana lakini anaishi sana katika bahari, yaani ulimwengu wa chini ya bahari. Alikuwa ni wakala mkereketwa wa Malkia wa Pwani(Queen of the Coast) na alikuwa muovu sana. Yeye aliwachukia Wakristo sana na alikwenda mwendo mrefu kupambana na Ukristo. Mimi nilikutana naye kwa mara ya kwanza wakati wa ziara yangu ya baharini ya kwanza. NINA alikuja kwa ajili ya kazi ya Malkia wa Pwani.

Tuliondoka mara moja na nilipofika pale chini niligundua kuwa tutafanya kikao na Lucifer/Shetani. Shetani, katika mkutano huu, alitupa maelekezo yafuatayo: Kupambana na waamini na sio wasioamini, kwa sababu wasioamini hao tayari ni wake. Baada ya kusema hayo, mmoja wetu akseliza swali: "Kwa nini?" Akasema sababu ni kwamba Mungu alimfukuza nje ya 'mahali' pale (alikataa kuita neno' Mbinguni 'na katika muda wote katika mikutano yetu tuliyofanya pamoja naye hakuwahi kutaja neno 'Mbinguni'. Badala yake alitumia neno 'mahali pale') kwa sababu ya kiburi, na kwa hiyo yeye **hataki Mkristo yejote afike huko (Mbinguni)**.

Pia alituambia kwamba hatupaswi kupambana na wanafiki. "Wao ni kama mimi," alisema. Aliendelea na hotuba yake na akasema: "Tunapaswa tu kupambana na Wakristo halisi" Kwamba wakati wake umekaribia, kwa hiyo tunapaswa kupambana kama vile haijawahi kutokea na kuhakikisha kwamba hakuna anayeingia mahali pale: "Sasa mmoja wetu akasema tumesikia kwamba Mungu alimtuma mtu kuwaokoa watu warudi kwa Mungu" Shetani kisha akseliza: "nani huyo?" mjumbe mmoja akajibu "Yesu" na kwa mshangao mkubwa, Lucifer akaanguka katika kiti chake. Akapiga kelele kwa mtu huyo na akamuonya kamwe asilitaje jina hilo kwenye mikutano yetu

kama anapenda maisha yake. Ni kweli kwamba kwa jina la Yesu kila goti litapigwa (Flp. 2: 10), ikiwa ni pamoja na Shetani.

Baada ya tukio hilo akatupa sisi moyo na alituambia kwamba tusiwajali "hawa wakristo", kwamba yeze Lucifer atakuja hivi karibuni kutawala dunia na atatupa,sisi mawakala wake, mahali bora ili tusihadhiriike/tusitaabike sawa na wengine duniani na yeze atatusfanya sisi watawala. **Aliendelea kusema kwa kuwa mwanadamu anapenda mambo ya kushangaza na ya ajabu, ataendelea kutengeneza mambo hayo na kuhakikisha kwamba mwanadamu hana muda kwa ajili ya Mungu wake na kwamba atatumia yafuatayo kuharibu kanisa:**

- 1.fedha,
- 2.mali,
- 3.Wanawake.

Mwishoni mwa hotuba hii akafunga Mkutano. Mkutano huo ndio uliokuwa wa kwanza kwangu mimi kukutana na Shetani. Mingine kadhaa ilifuata baada ya mkutano huu. Tulipokuwa tukiondoka, Malkia wa Pwani, ambae sasa alionekana katika maumbo mbalimbali, alinialika mimi na nyumbani mwake. Aliingiza majivu ya binadamu pamoja na vitu vingine ndani ya mifupa yangu ya miguu yote, jiwe (si jiwe la kawaida) katika kidole changu na kitu kingine ndani ya mfupa wa mkono wangu wa kulia.

Kila moja ya vitu hivi ilikuwa na kazi yake. Jiwe katika kidole changu ilikuwa ni kwa ajili ya kujua mawazo ya mtu ye yote dhidi yangu. Moja katika mkono wangu wa kulia ilikuwa kuniwezesha mimi kuharibu na yale yilio katika miguu ni kwa ajili ya kufanya miguu yangu kuwa migumu zaidi na kuifanya kuwa hatari zaidi na pia kuniwezesha mimi kubadilika na kuwa mwanamke, mnyama, ndege, paka, nk Alinichukua mpaka kwenye moja ya maabara na akanipa darubini, TV na video. Hivi havikuwa vitu vya kawaida lakini vilikuwa vinatumika katika kuchunguza Wakristo waliozaliwa mara ya pili na waendaji tu wa kanisani ndani ya kanisa.

Mwishowe alinipa wasichana kumi na sita wa kufanya nao kazi. NINA alikuwa ni mmoja wao. Nilikuja tena Lagos nikiwa na zawadi hizo nilizozitaja hapo juu.

Kugeuzwa kuwa wakala wa shetani

Sikuwa na hisia za kibinadamu wala huruma katika moyo wangu tena. Nilikwenda katika utekelezaji mara moja na niliharibu majengo matano kwa mpigo. Zote zilizama ndani ya ardhi na wenyeji wao. Hii ilitokea Lagos mwaka Agosti 1982. Mkandarasi aliwajibika kwa kutoweka msingi mzuri na alilipa haswa kwa hili. Uharibifu mwingu unaotokea hivi leo katika dunia si kwamba wote umesababishwa na mwanadamu. Wajibu wa shetani ni kuiba, kuua na kuharibu. Nasema tena, "Shetani hana zawadi ya bure".

Nilikwenda kusababisha ajali katika barabara n.k. Kisa ninachopenda kusimulia ni kuhusu kijana mmoja aliyejewa ndio ameokoka tu ambae alikwenda akishuhudia wokovu wake na ukombozi alioupati. Alikuwa anasababisha madhara mengi katika ulimwengu wa roho kwa ajili ya kufanya hivi, hivyo nilipanga kufanya ajali kwa ajili yake. Siku moja alikuwa kwenye basi zuri sana akienda Lagos. Alikuwa ameitwa ili aje kutoa ushuhuda wake. Basi lilipokuwa katika mwendo wa kasi, mimi nikalizungusha tairi nje ya barabara hivyo likaenda na kugonga kwenye mti. Abiria wote walikufa isipokuwa huyu kijana.

Kupona kwake ilikuwa ni kimuujiza kwa sababu alitoka nje ya gari kupitia buti ya basi na kupiga kelele: "niko salama! niko salama! "Tulijaribu kumzuia asishuhudie lakini tulishindwa.

Kwa njia ya TV, tunaweza kujua mtu aliyetubu, mpya na tunamfuatilia kwa ukaribu kuona kama tunaweza kumfanya akarudi nyuma. Kama baada ya miezi sita hatuwezi kufanikiwa, tunakwenda katika biashara yake na

kuifanya iwe mufilisi. Kama ye ye ni mtumishi wa umma tutamnyanyasa kupertia kwa bosi, na kama inawezekana tunafanya bosi kusitisha mkataba au uteuzi wake. Kama baada ya haya yote hawezi kurudi nyuma basi tunaachana nae. Lakini kama atarudi nyuma anauawa kuhakikisha kwamba hapati nafasi ya pili kutubu.

Niliharibu maisha kwa kiasi kwamba Lucifer akafurahishwa na kunifanya niwe mwenyekiti wa wachawi. Mwezi mmoja baada ya Uenyekiti wangu, mukutano uliitishwa. Tulihudhuria mukutano huo kama ndege, paka na nyoka. Viumbe hawa hutumiwa kwa ajili ya sababu zifuatazo:

1. Kuwa ndege kunafanya wachawi wawe hatari zaidi.
2. Kuwa paka kunafanya wachawi wawe na uwezo wa kuwa katika roho na binadamu.
3. Kuwa panya kunawawezesha wachawi kuingia katika nyumba kwa urahisi, kisha wakati wa usiku wanakuwa kivuli, na kisha binadamu na kunyonya damu za watu.

Katika mukutano huo tulikuwa na agenda moja tu: "**Wakristo**" Tukapanga kuitisha mukutano wa Afrika wa wachawi mjini Benin mwaka 1983. Tulichapisha katika magazeti yote ya kila siku na vyombo vyote vya habari vya umma. Nguvu zote za giza walijipanga na walikuwa na uhakika sana kwamba hakuna kitu chochote kitakachoingilia kwa kupinga mukutano huu. Kwa kweli kila kitu kilipangwa vizuri na kulikuwa hakuna mwanya.

Ghafla, Wakristo Nigeria wakaingia kwenye maombi na sifa kwa Mungu wao na mipango yetu yote ilizimwa. Si tu kwamba mipango yetu ilizimwa peke yake lakini pia kulikuwa na mtafaruku haswaa katika ufalme wa giza. Matokeo yake, mukutano wa wachawi 'na mapepo haukuweza kufanya Nigeria. Wakristo wanapaswa kutambua kwamba wakati wao wanaingia ndani katika sifa halisi kwa Mwenyezi Mungu, kunakuwa na shida na mvurugano kote ndani ya bahari na angani, na mawakala wa shetani wanakuwa hawana nafasi ya kupumzika/kutulia. Maombi ni kama kutupa bomu la kushitukiza katikati yetu na kila mta anatoroka kuokoa maisha yake.

Kama Wakristo wakitambua na kutumia nguvu na mamlaka ya Mungu aliyowapa, wataweza kudhibiti mambo ya taifa lao! Wakristo tu ndio wanaonaweza kuokoa taifa letu.

Baada ya mukutano huu kushindikana, ambao baadae ulifanyika nchini Afrika Kusini, niliitwa tena baharini. Nilipofika, niliambiwa kutokea wakati huo nilitakiwa kufanya bahari kama nyumbani kwangu na kutembelea dunia kwa shughuli ngumu tu. Nilipewa kazi mpya: kubuni hirizi za waganga, nikiwa mhusika mkuu wa chumba na mtumaji wa zawadi, yaani ufunguzi wa makanisa (nyumba za maombezi), ufunguzi wa nyumba za kujifungua, kufungua maduka na kufanya yafanikiwe, kuwapa 'watoto na fedha. Haya yataelezwa moja baada ya jingine:

1. Ufunguzi wa "Makanisa ya nguo nyeupe":

Wakati mta anakuja kwetu kwa msaada wa kujenga nyumba ya maombi na kumsaidia kufanya uponyaji nk, basi atapewa baadhi ya sheria:

- a) Atakubali kuchangia kwetu nafsi moja au mbili kila mwaka.
- b) Katika ngazi fulani ya ofisi katika kanisa mta atakuwa anaunganishwa na jamii yetu.
- c) Hakuna mwanachama angeruhusiwa kuja katika nyumba ya maombi na viatu mguuni.

Akisha kubali matakwa hayo, **atapewa kitu changarawe nyeupe, mifupa ya binadamu, damu na hirizi, vyote katika chungu**. Atapewa maelekezo ya **kuzika chungu hiki na vitu vyake vyote mbele ya kanisa na atazika msalaba juu yake**. Baada ya maziko msalaba tu ndio unapaswa kuonekana. Atashauriwa **kujenga Bwawa au kuweka basini ambapo roho chafu zinaendelea kuweka maji maalum. Maji haya ndiyo unasikia huyaita "maji matakatifu."**

Watu wengi wakisumbuliwa na roho mbaya wanakwenda kwa hawa "manabii" kwa ajili ya kuwafukuza. Ukweli ni kwamba, wao huongeza mapepo zaidi kwao. **Shetani hawezi kumuondoa nje shetani.** (Luka 11:17-19) Kile

nabii atakifanya ni, atamuombea mshirika na kisha atampa mshirika kitambaa chekundu ili kuweka katika nyumba yake, na kisha atamshauri awe anaomba akiwa na mishumaa na uvumba. Kwa kitendo hiki mtu anatalika sisi kwenye nyumba yake. Wakati mwininge mshirika anashauriwa kuleta mbuzi n.k, kwa ajili ya sadaka. Sadaka hizi ni kwa ajili yetu kuja na kusaidia kumtibu mtu huyu. Nabii hana uwezo wa kutibu au kuponya

2. Ufunguzi wa Maternities (sehemu za kujifungulia):

Kama mwanamke anakuja kwetu kwa ajili ya kupata msaada wa kufungua kituo cha uzazi na kukifanya kifanikiwe, atapewa sheria zifuatazo:

"Mwezi utachaguliwa ambao watoto wote wanaozaliwa katika mwezi huo kwenye kituo hicho watakuwa, na miezi mingine watoto wataishi."

Kama atakubali basi atapewa, dawa ambayo itawavutia watu kuingia katika kituo hicho cha uzazi. Kuna maternities kama hizi Onitsha, Lagos, nk viatu haviruhusiwi katika vituo hivyo.

3. Ufunguzi wa Maduka ya dhana:

Mtu anapotufuata sisi kwa ajili ya msaada katika suala hili, anapewa pete na mashariti kwamba hakuna mwanamke atakayeruhusiwa kugusa pete yake. Ni lazima pia akubali kuwa mwanachama wetu. Kama atakubali kupokea kutimiza masharti hayo, duka lake litakuwa linajaa vifaa vya ubora na vya kisasa.

4. Kutoa Watoto

Kama mwanamke tasa atakwenda kwa mganga, baada ya kuweka malalamiko yake, ataulizwa kuleta yafuatayo: jogoo mweupe, mbuzi, chaki ya asili na baby care. Ataambiwa arudi na atakapokuwa ameondoka,mganga atakuja kwetu kuleta vitu hivi. Kisha tutachanganya vitu fulani ambavyo ni vigumu kuelezea kwa maandishi, na tutaweka majivu ya mwanadamu. Atatumia dawa hii kumpikia chakula mwanamke nk. Atapata mimba na kuzaa, lakini siyo binadamu wa kawaida. Kama mtoto ni wa kike atawenza kuishi na hata kuolewa lakini atakuwa bado tasa maisha yake yote. Kama mtoto ni wa kiume ataishi lakini atakufa kifo cha ghafla. Huwa awaishi kuzika wazazi wao.

Napenda kukueleza hapa kwamba utasa mara nyingi unasababishwa na mapepo. Unaweza kuona mwanamke tasa hapa duniani, lakini anawenza kuwa na watoto wengi tu baharini. Kwa hiyo nashauri watoto wa Mungu kumsubiri Mungu pekee kwa sababu Mungu tu ndio huwapa watu watoto halisi.

5. Kutoa fedha:

Kama mtu anakuja kwetu kwa ajili ya kupata fedha, atapewa masharti yafuatayo kuyatimiza: Ataambiwa kutoa sehemu ya mwili wake au kama ana familia ataambiwa kuleta mtoto wake wa kiume. Kama yuko mwenyewe basi ataombwa kumtoa kafara kaka yake au mdogo wake.

Yeyote atakayeamua kumleta ni lazima atoke katika tumbo moja. Kitu muhimu cha kutaja: siku ya kufanya mauaji ya mhusika, mtu ambaye amempeleka atapewa mkuki,au mshale. Uhushiano wake utawekwa katika file kwenye kioo. Mara baada ya mtu yule anayetakiwa kumtoa kupita, ataambiwa apige ile sehemu ya faili iliyoko kwenye kioo,basi akifanya tu hivi yule mtu anakufa pale mahali alipo.

Kuna njia nyingine lakini jambo moja Shetani hufanya ni kwamba: anahakikisha kwamba katika njia hio tofauti, mtoaji anakuwa mwajibikaji kwa ajili ya kifo cha mwathirika, kwa kufanya mtoaji ampige mlengwa, kumbuka **Shetani hana zawadi ya bure!**

Sura 4: Jinsi shetani anavyopigana na Wakristo

«Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. »
Waefeso. 6: 10-12

Kupigana na Wakristo

Baada ya amri ya Lucifer kupambana na Wakristo, sisi tuliketi na kuchora ramani ya kupambana nao kama ifuatavyo:

1. Kusababisha magonjwa.
2. Kusababisha utasa.
3. Kusababisha usingizi katika kanisa.
4. Kusababisha machafuko katika kanisa.
5. Kusababisha uvuguvugu katika kanisa.
6. Kuwafanya wawe wajinga wa neno la Mungu.
7. kwa mitindo na uigaji.
8. Kupambana nao kimwili.

Miongoni mwa hayo juu napenda kuwaeleza mawili:

1. Kupambana kimwili:

Kwa TV niliyopewa, niliwaona Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Hatupigani na wanafiki kwa sababu wao ni mali yetu tayari. Tuliweza kuwatuma wasichana wetu kwanza katika makanisa makubwa. Ndani ya kanisa walikuwa wanatafunu jojo au kumfanya mtoto alie au kufanya chochote ambacho kilivuruga watu kusikiliza neno la Mungu. Wanaweza kuamua kuja kiroho na kusababisha watu kulala wakati mahubiri yanaendelea. Wakikuona uko makini kwa sababu ya mahubiri, wanaweza kukusubiri nje ya kanisa na unapokuwa ukitoka kuja nje ya kanisa, mmoja wao anakusalimu na hata kukupa zawadi (na mara nyingi ni zawadi ya kitu kile upendacho) na wataonekana ni marafiki sana. Atafanya kila kitu na kabla haujajua kinatokea unakuwa umesahau kila kitu ulichojifunza kanisani . Lakini kwa Mkristo halisi,mmoja ya wasichana hawa ,baada ya ibada, ataruka nje kukusalimu na atapenda kujua nyumba yako kwa kisingizio kwamba ye ye ni mgeni katika mji na hawajui Wakristo wengi wanaomzunguka. Ukimpeleka nyumbani kwako, kwa haraka atanunua ndizi na Mkristo atachukulia hii kama ishara ya upendo. Ataendeleza ziara zake mpaka hatimaye anaweka mbali mwanga wa Kristo ndani yako na kisha anaacha kuja. Shughuli kuu katika makanisa yaliyo hai na shirika zilizo hai ni : kuwasumbua Wakristo wasisome na kujifunza neno la Mungu, na hivyo kuwafanya wajinga wa mamlaka na ahadi za Mungu. Katika mikutano ya injili wasichana hawa wanatumwa kusababisha kutolewana na ugomvi.

Jinsi wakirsto wanavyojulikana?

Wakristo waliozaliwa mara ya pili hawajulikani kwa Biblia wanayobeba kila siku au ibada nyingi wanazohudhuria. Wanajulikana katika ulimwengu wa roho kwa mwanga ambaa huendelea kuangaza wakati wote kama mshumaa mkali sana katika moyo au mduara wa mwanga unaozunguka kichwa au ukuta wa moto unaowazunguka. Mkristo anapokuwa akitembea, tunaona malaika wakitembea pamoja naye mmoja mkono wa kuume, mmoja kushoto, na mmoja nyuma. Hii inafanya kuwa vigumu kwa sisi kuja karibu yake.

Njia pekee ya sisi kufanikiwa ni kwa kumfanya Mkristo atende dhambi, na hivyo anatoa mwanya wasisi kuja na kuingia ndani. Mkristo akiwa anaendesha gari na tunapotaka kumdhuru, tunaona kwamba siku zote hayuko peke

yake katika gari. Siku zote kuna malaika pembeni mwake. **Oh kama Mkristo akijua tu yote ambayo Mungu anafanya kwa ajili yake, hawezi kutenda dhambi au kuishi ovyo ovyo !**

2. The Making of Backslidden Christians

Kama mwenyekiti aliyeetuwa na Lucifer, niliwatura wasichana hawa makanisani na sharika zinazoishi/hai . Wasichana hawa wanakuwa wamevalia vizuri na baada ya mahubiri wanakuja kwenye madhabahu kama wameitwa, na watajifanya kuwa wamempokea Kristo na wataombewa. Mwishoni mwa ushirika au ibada watazungukazunguka nje na kumsubiri mhubiri ambaye kiukweli atakuwa na furaha sana na waongofu hawa wapya.

Waongofu hawa wapya wanaweza hata kumfuata mhubiri nyumbani kwake. Kama mhubiri hana roho ya kupambanua watamvutia aingie katika dhambi ya uzinzi au uasherati . Hii inafanyika wakati pale mhubiri anapokuwa amemtamani. Atahakikisha amendelea katika dhambi hii mpaka pale atakapoona amemzimisha Roho wa Mungu ndani yake na kisha anaondoka, huku **mkakati wake umetimia**.

Mahali hapa ningependa kutoa ushuhuda wa Mhubiri. Katika ulimwengu wa roho/kipepo yeye anajulikana kama mtu wa Mungu(man of God). Anapokwenda kwenye magoti yake kunakuwa na mvurugano kati yetu. Kwa hiyo tunatuma wasichana hawa kwake. Mtu huyu anaweza hata kuwalisha lakini atakataa kunaswa na mitego yao. Walijaribu kila walivyoweza lakini kamwe hawakuwahifanikiwa. Matokeo yake, wasichana hawa waliuawa kwa kushindwa kwao.

Mimi nilijigeuza na kuwa mwanamke kisha nikamwendea, kwa maneno na vitendo nilijaribu kumshawishi, lakini alikuwa mgumu. Hii ilikuwa ni kazi kubwa mno kwangu, hivyo nilidhamiria kumuua kabisa kimwili. Siku moja, Mhubiri huyu alikwenda soko la barabara ya Oduekpe. Nilimwangalia na alipoinama chini kununua baadhi ya bidhaa nilijizungusha kwenye tairi za trailer iliyokuwa imebeba mafuta ya mafuta kuelekea sokoni alipokuwa mhubiri. Trailer/gari likapiga nguzo kubwa sana ya NEPA na ikangukia katikati ya soko, na kuacha watu wengi wamekuwa, lakini Mhubiri alitoka mzima. Jinsi gani alipona ulikuwa ni muujiza. Siku nyingine, nilimuona akisafiri kwenda Nkpor kwa miguu. Nililizungusha gari la jeshi lililokuwa limebeba viazi vikuu vya kumuua. Lori lilikwenda moja kwa moja ndani ya barabara mpya ya makaburini, na kuwaua watu wengi mno, lakini muhubiri huyu bado alikuwa mzima. Baada ya jaribio hili la pili tulikata tamaa. Yeye bado yuko hai hata leo hivi!

Kwa sababu ya mkristo mmoja, shetani anaweza kuamua kuharibu roho nyingi, akifikiri anaweza kumuua, lakini siku zote anashindwa. Matukio haya yameyotokea kwa Wakristo wengi bila ya wao kujua, lakini Mungu wao huwaokoa mikononi mwa adui zao siku zote. Shida ni kwamba, Shetani hachoki. Mawazo yake yako palepale: "Ninaweza kufanikiwa." Lakini kamwe hafanyikiwi. kama tu Mkristo atatembea na **Upendo wa Mungu na kubakia ndani yake na ajichanganyi na mambo mengine ya maisha haya, shetani hawezi kumpata, vyovoyote vile shetani anaweza kujaribu. Wasioamini tu ndio wako chini yake.**

Ukandamizaji wa Wakristo

Hii hutokea hasahaha katika ndoto. Mkristo anaweza kuona katika ndoto yake yafuatayo:

1. Mtu mfu anamtembelea
2. Kinyago kinamfuata.
3. Marafiki wanaogelea katika mto
4. Marafiki wanaleta chakula na wanamsihi ale.
5. Msichana wa kike anafanya ngono au msichana aliyeolewa anafanya mapenzi na mwanaume. Hii, kama si haitashughulikiwa, wakati mwingine husababisha utasa.
Au mwanamke mjamzito anajiona anajamiiiana na mtu. Hii, kama haikushughulikiwa, inaweza kusababisha kuharibika kwa mimba.

Kama Mkristo akikutana na hayo huu katika ndoto yake, hatakiwi kuweka kando mambo haya kwa kupuuzia bali akitoka kwenye ndoto tu inampasa ajichunguze mwenyewe na atubu dhambi yejote ile inayojulikana na kufunga pepo wote na kumsihi Mungu arejeshe kila kitu alichokutana nacho ndotoni. Hii ni muhimu sana. Mtu ni lazima pia kutafuta msaada na ushauri kwa mkristo aliyejazwa na Roho Mtakatifu, wakongwe katika imani.

Shetani na mkakati wa kuvuna roho

Yesu Kristo alipokuwa akiondoka duniani, aliwapa wanafunzi wake amri: "Akawaambia enendeni ulimwenguni kote mkafanye wanafunzi kwa kila taifa" Wakati Wakristo bado wanasubiri mazingira mazuri na wakati mzuri kwa ajili ya kutii amri hii, Tofauti ni kwamba, **mawakala wa shetani wako na bidii kubwa zaidi katika kuvuna roho za Wakristo !**

Moja ya maeneo ya shetani katika kuvuna roho ni shule za sekondari, hasa za wasichana. Baadhi ya wasichana wetu wanatumwa katika shule kama wanafunzi. Tunawapa kila chupi ya kisasa na nzuri na zenye gharama kubwa. Hii ndio kipaumbele cha kwanza, kwa sababu katika hosteli za wasichana wao hupendelea kutumia chupi tu . Mawakala wetu kamwe hawakosi kitu chochote, vipodozi, nguo , chupi , vitabu, fedha na mahitaji. Sabuni maalumu za kuoga atapewa ili kutoa kwa mwanafunzi yejote ambaye atahitaji sabuni kutoka kwake. Msichana anayetaka kuwa kama yeje atavutiwa na kufanya urafiki nae. Hatua kwa hatua wakala wetu atatutambulisha kwake. Nasi tutamtembelea kimwili na kuanza kumpa zawadi na kumtimizia mahitaji yake. Kwa hili, atajunga nasi kwa hiari . Yeye naye atawavuta wengine na itaendelea hivyo. Hii inachukuliwa kama mkakati wenye dhamira ya kufanikiwa.

Jambo moja la kuzingatia: shetani hamlazimishi mtu yejote. Anachokifanya ni kuwavutia watu na kuwafanya waje kwake kwa hiari. Ndiyo maana Biblia inasema: "mpingeni shetani naye atawakimbia" (James 4:7). Eneo jingine la kuvuna roho la shetani ni kutoa lifti. Tunawapeleka wasichana wetu kusimama barabarani, na kwa kawaida huwa ni warembo sana na wamevaa mavazi ya kuvutia. Unaweza pia kuwapata kwenye hoteli na kupitia maeneo haya tunawapata wanaume na wanawake. **Watu wengi tunaowaona wanatangazwa katika magazeti kama wamepotea, ni baada ya kutoa lifti kwa wasichana, wasiowajua.**

Unapaswa kuwa makini ni nani ambaye unampa lifti.

Sura 5: Nilipokutana na Yesu

Katika mwezi Februari 1985, tulikuwa na mukutano wetu wa kawaida katika bahari, baada ya hapo niliamua kusafiri kwenda Port Harcourt katika jimbo la Rivers, kutembelea mke wa marehemu mjomba wangu. Nilikutana na mtu mmoja aitwaye Anthony. Yeye ana karakana pale kwenye makutano ya Nwaja, sambamba na barabara ya Trans-Amadi, Port Harcourt, Rivers State. Alimtuma mtu huyu kwa ajili yangu na kwa sababu katika jamii yetu tuna sheria kwamba hatupaswi kukataa munto, niliamua kujibu munto wake. Nilikwenda kwake mchana siku ya Alhamisi ya wiki hiyo. Alianza kwa kusema Mungu amempa ujumbe kwa ajili yangu. Akatoa Biblia yake na kuanza kuhubiri. Kulikuwa na Wakristo wengine watatu wameketi (mwanaume na wanawake wawili). Aliendelea na mahubiri yake kwa muda mrefu na sikuwa na uhakika kama nilisikia yote aliyosema. Alinisihi nipige magoti kwa ajili ya maombi. Nilimitii na taratibu nikapiga magoti.

Mara ghafla akaanza maombi yake. Naliangushwa chini na roho wa Mungu na nikaanguka nikajinyoosha. Nilijitahidi kuinuka na nikasimama kama chuma. Nikavunjavunja viti vyta chuma ndani ya karakana. Niliangalia nje na kuona wanachama watatu wa jamii yetu ya siri, mwanaume na wasichana wawili. **Walikuja katika umbo la binadamu na kusogea mpaka mlangoni lakini kwa sababu ya nguvu ya Mungu hawakuweza kuingia.**

Nina hakika kengele ndani ya bahari iliwataarifu shida ilipokuwa na kwa TV walijua wapi ambapo tatizo lilikuwa na walituma waokoaji wasio na nguvu. Hii mara zote hufanyika wakati mwanachama yeoyote ameingia katika matatizo. Wakati wale wakristo wawili wakinivuta chini kwenye magoti yangu, wasichana wawili waliendelea kuomba na kufunga mapepo, lakini hawakuwa wanalenga hasa nini wanachofunga. Wakaniuliza kama ninamuamini Yesu Kristo, sikusema chochote. Wakaniuliza niite jina la Yesu, nami nilikataa. Wakaniuliza jina langu niliwaambia. Wakajitahidi kwa masaa na wakaniachia niende. Hakuna roho iliyondolewa ndani mwangu, hivyo nilitoka hivyo hivyo sawa na nilivyoingia.

Maatukio ya Kanisani

Siku iliyofuata ilikuwa ni Ijumaa, nilialikwa na Anthony huyo huyo kuhuduria usiku wa mkesha wao katika kanisa la Assemblies of God, Silver Valley, Port Harcourt. Nilikubali mwaliko huu kwa sababu kuhuduria ibada ya makanisa na kusababisha usingizi na machafuko ilikuwa ni sehemu ya kazi yetu. Ibada ilianza na pambio. Tuliimba mpaka mmoja wa wajumbe wenzangu akaanzisha kiitikio maarufu cha bendi moja ya kikristo, kinachozomea uwezo na mamlaka ya nguvu zingine isipokuwa nguvu za Yesu.

Kisha nikaanza kucheka. Nilicheka kwa sababu katika roho niliwaona maisha yao karibu robo tatu ya watu waliokuwa wanaimba kiitikio kile walikuwa wanaishi katika dhambi. Nilijua kuwa **kwa sababu ya dhambi katika maisha yao, ni wazi kuwa wangeharibiwa vibaya na nguvu hizi. Ni muhimu kwa wakristo kutii neno la Mungu na si kuruhusu dhambi kubaki katika maisha yao.** Katika ibada hiyo tulikuwa wanne kutoka baharini na tulikuwa tukiimba na kupiga makofi pamoja nao. Tena nataka kusisitiza hapa kwamba wakati ibada inaanza, waumini ni vyema na wanashauriwa kwanza kukiri dhambi zao na kutubu, kisha kwenda katika kipindi cha sifa halisi kwa Mungu. Hii itafanya wakala wa Shetani awe na wasiwasi sana na ataondoka ili kuyaokoa maisha yake.

Katika ibada hii tulikuwa tunaujasiri sana hata tukaingia katika utendaji. Wengi walianza kulala, pambio zilikuwa zikiimbwa kwa udhaifu na mambo yakaenda zig-zag. Ndugu Anthony alikuwa tayari amewaambia kuhusu mimi kwa hiyo saa 02:00 waliniita nitoke mbele na waanze kuniombea. Mara nilipotoka mbele walianza kuita damu ya Yesu. Nikawasimamisha na kusema: "Si kuomba kwa damu ya Yesu ndio ufumbuzi. Mimi ni mwanachama mkubwa sana katika jamii za watu wa chini ya bahari. Kama mnakubali kwamba mnawenza kunikomboa, basi nipige magoti. "Maneno haya niliyasema sikuwa nimeyapanga. **Damu ya Yesu inaogopesha mapepo na**

kumlinda muamini, lakini haifungi mapepo. Kufunga mapepo na kuyatoa inafanyika tu pale Mkristo anapotumia mamlaka yake na kutoa amri.

Walikubaliana na mimi nikapiga magoti. Katika hatua hiyo dada mmoja aliongozwa na Roho wa Mungu na kuongea kwa sauti akasema: "Kama hauko vizuri, usijaribu kusogea karibu!" Nina uhakika wengi hawakuwa wameelewa nini maana yake. **Ni hatari kwa Mkristo anayeishi katika dhambi kutoa pepo.** Wengi waliondoka na wachache wakatoka kuja kuomba kwa ajili yangu. Walipoanza kusema "Katika jina la Yesu," Nikasikia (impasuko mkubwa) big bang kubwa ndani yangu na nikaanguka juu ya sakafu. Mara pepo wanaokuruka ndani yangu wakanza kufanya kazi. Nikaanza kukimbia kwa kifua changu. Mtu yejote mwenye hili pepo la kuruka ni muovu na hatari sana. Ndugu/Waamini hawakuona nini kinatoka kiroho. Nilikuwa nakimbia mbio kwa sababu ya nguvu kubwa iliyokuwepo katika chumba.

Nguvu mbili za upinzani zikaanza kufanya kazi pia na anga likabadilika. Ghafla nikasimama na nikawa na vurugu sana nk. Pepo, likatoka ndani yangu na kumkamata mvulana aliyekuwa kati yao na likaanza kupambana nao, likijaribu kuniokoa mimi. Ndugu hawakupoteza muda nae badala yake wakamkamata yeye pamoja na wengine waliokuwa wanaogopa na kumfungia katika vestry ya kanisa. Hii iliendelea mpaka 7:00 Nilikuwa nimechoka sana kimwili na nikawa nimetulia, hivyo ndugu wakakusanyika karibu yangu tena na kuanza kuniambia: Wataje ni akina nani hao nk Nilikaa kimya tu. Baada ya kusubiri kwa muda mrefu na kuona sikuwa nimesema kitu, walidanganyika na kuamini kwamba nilikuwa nimekombolewa. Wakaomba na tukatawanyika. Nilikuwa kimwili dhaifu kiasi kwamba ilikuwa ni vigumu kutembea kwenda hata nje ya kanisa.

Lakini kitu fulani kilitokea, mara baada ya kwenda nje ya kanisa na kuvuka barabara, nikawa na nguvu nyingi za kimwili. Labda inawezekana baadhi ya mapepo yaliyotoka yakarudi tena ndani yangu. Nilikasirika sana na kuamua kulipiza kisasi juu ya kanisa. "Hawa watu wamenidhalilisha" Nikajisemea mwenyewe, na kwa jinsi walivyofanyia nitarejea Lagos na kupata nguvu zaidi pamoja na wengine waovu kama mimi, na kisha narudi Port Harcourt kulipiza kisasi kwa kanisa zima la Assembly of God, Silver Valley.

Safari yangu ya Lagos

Nilipofika kwenye nyumba ya mke wa mjomba wangu, Niliwaambia nitaondoka kurudi Lagos mara moja. Nilikataa wasinisihi kubaki na nikachukua teksi mpaka kituo cha magari cha Mile 3. Ambapo nilichukua teksi ya kwenda Onitsha. Nia yangu ilikuwa kusimama Onitsha, kumuona rafiki na kisha kuendelea mpaka Lagos. Pale Mile 3 tukaondoka na tulipokuwa tumefika njia panda ya kwenda Omagwe, katika makutano ya uwanja wa ndege wa Kimataifa, nikasikia sauti ikiniita kwa jina langu la asili "NKEM." Nikageuka nyuma kuona kama kuna sura yeyote ninayojua kwenye teksi, lakini hakukuwa na mmojawapo anayenijua. Huyu anaweza kuwa nani? Ni marehemu mama yangu tu ndiyo alikuwa akiniita kwa jina hilo, wengine wote pamoja na ulimwengu wa kipepo walinjua mimi kama Emmanuel.

Nilipokuwa bado nashangaa, sauti ikasikika tena : " **NKEM , unakwenda kunisaliti kwa mara nyingine tena ?**" Sikuweza kuitambua sauti lakini sauti iliendelea kuniuliza : " **Je, unakwenda kunisaliti kwa mara nyingine tena**" Ghafla nikawa na homa kali. Joto lililotoka mwilini mwangu ilikuwa liko juu mno kiasi kwamba abiria wengine walilisikia. Mmoja wao akanuliza: "Mheshimiwa, ulikuwa vizuri kabla ya kusafiri?"Niliwaambia nilikuwa vizuri na sikuwa naumwa hata na kichwa kabla ya kuondoka Port Harcourt.

Tulipofika Umuakpa Owerri, nilianguka ndani ya teksi. Kilichofuata ni kwamba watu wawili, warefu na wakubwa, walikuja kunichukua mmoja upande wa kushoto na mwingine upande wa kuume, na hawakuzungumza neno lolote kwangu. Waliniongoza kwenye barabara mbaya sana yenye chupa na vipande vyta chuma vilivyokuwa vinanikatakata nikaanza kulia, lakini hawa watu hawakusema neno lolote. Tuliendelea mbele na kufika kwenye barabara ya kasi. Ilikuwa hapa mmoja akaniambia "**Wewe unatafutwa sana**"na tukaendelea. Tuliendelea mpaka

jengo moja kubwa na refu lililofanana na jengo la mikutano. Tulipokanyaga ndani ya sakafuni tu sauti kutoka ndani ikasema: "**Muingizeni ndani**" Waliniingiza ndani kisha wakatoweka, na kuniacha peke yangu.

Nilichokiona ndani ya ukumbi huu ni vigumu kueleza, lakini nitajaribu kueleza kadiri nitakavyoweza. Ukumbi ulipambwa vizuri sana na ulikuwa mkubwa sana na mrefu kiasi kwamba ilikuwa ni vigumu kuona mwisho wake. Nilitembea mpaka katikati na ndipo niliweza wa kuona mwisho wake. Mwishoni kulikuwa na madhababu. Kisha nikaona kiti cha enzi na na aliyekuwa ameketi juu ni mwanaume mzuri sana mwenye nguo inayong`aa kama jua. Akasema: "**Njoo!**" Lakini kwa sababu ya mwangaza wake sikuweza kwenda. Kila nilipojaribu kunyanya mguu wangu nilianguka.

Nilisimama, nikajaribu tena na nikaanguka. Ghafla mtu huyo akatoka kwenye kiti cha enzi alipokuwa amekaa, akahamia kwa juu kidogo nilipokuwa nimesimama. Kisha mikono miwili ikatoka nje ya mtu huyo, ikanishika kichwa changu na kunitikisa na mwili wangu wa kibinadamu ukajivua kama unavua nguo.. Na yule mimi mwenywewe sasa akasimama. Mikono akaikunja kama mtu anaye kunja nguo na akaitupa kwenye kona. Mtu yule akarudi tena kwenye kiti chake cha enzi na akakaa na kusema tena: "**Njoo!**"

Kutakaswa Kiroho

Nikatembea mpaka pale naye akasogea kutoka katika kiti cha enzi, akanyofoa mguu yangu mmoja baada ya mwingine na akamwaga kile kilichokuwa ndani yake, na akaiweka tena vizuri. akafanya hivyo pia kwenye mikono na akaiweka tena, Yaani ni hivi sehemu zote ambazo Malkia wa Pwani aliweka nguvu zake humo. Nikatafakari sana kwenye fikra zangu, huyu atakuwa nani na amejuaje kuwa maeneo haya ndiyo yalikuwa yametunza nguvu zangu. Baada ya haya alirudi tena kwenye kiti chake na akanimbria niende. Nilipoanza tu kutembea, vitu fulani vikaanza kuanguka kutoka kwenye mwili wangu , magamba yakaanguka kutoka katika macho yangu, nk, lakini kabla sijafikia madhababu tayari vikaacha. Aliniuliza. "**UNAKWENDA WAPI ?**"

Nikajibu, nikasema, "Ninaenda Onitsha kumuona rafiki." Akasema: "**Ndiyo, lakini mimi nitakuonyesha nini ulichopanga kwenye akili yako.**" Hadi wakati huu sikujua alikuwa ni nani, lakini jambo moja nililokuwa na uhakika nalo ni kwamba alikuwa mwenye nguvu zaidi kuliko nguvu zote nilizowahi kukutana nazo. Alisema kwa ishara na mtu ambaye aliamriwa kunionyesha mimi nini nilichokuwa nimedhamiria moyoni kukifanya. Mtu huyu alinipeleka kwenye chumba na akufungua kitu kama ubao. Kwa kweli, kama kulikuwa na njia ya kutoroka ningeweza kutoroka, kwani mbele yangu yaliandikwa yote niliyopanga kufanya dhidi ya Wakristo na mpango wangu dhidi ya kania la Assemblies of God, Silver Valley. Mtu huyu akanileta tena madhabahuni na akanicha.

Akatoka katika kiti cha enzi na akanishika kwa mikono yake na akasema kuwa anakwenda kunionyesha mimi mambo fulani. Tulipokuwa njiani Akasema: "**Mimi sitaki wewe upotee lakini nikuokoe na hii ni nafasi yako ya mwisho. Kama hautatubu na kuja kunitumikia, utakufa.**" Nitakuonyesha makazi ya waliookolewa na waasi." Alivyosema hivyo, nikajua alikuwa ni **Yesu Kristo**.

Ufunuo wa Kimbingu

Tukaingia katika chumba fulani na akafungua kitu kama pazia. Niliona dunia nzima, watu na shughuli zote za kinachoendelea. Nikaona Wakristo na wasio wakristo wote wanafanya jambo moja au jingine. Tulikwenda kwenye chumba cha pili . Akafungua pazia tena na nilichokiona ilikuwa ni kitu mbaya kuonekana. Watu wamefungwa minyororo ! Aliwaita watu hawa " **wanafiki.** " Watu hawa walionekana ni watu wenye huzuni kubwa, Akasema: ". **Watabakia hivi mpaka siku ya hukumu "**

Tulienda katika chumba cha tatu. Akafungua pazia na nikaona watu wengi wanafuraha na wakiwa wamevaa mavazi meupe. Wakati huu nikamuuliza : " Ni kina nani hao " Akasema: "**Hawa ni wale waliokombolewa wanasubiri ujira wao.**" Tulikwenda katika chumba cha nne na nilichokiona kilikuwa cha kutisha mno.

Ndugu msomaji, ni vigumu kuelezea. Ilionekana kana kwamba mji mzima unawaka katika moto. Kuzimu ni halisi na niyakutisha. Kama ulikuwa umefanywa kuamini kwamba Mbinguni na Kuzimu ni hapa duniani na kwamba hakuna maisha mengine mara baada ya kifo bali ni kuoza na kupotea kabisa, ni bora ukashauriwa vizuri hapa na sasa kwamba kuzimu halisi ni halisi na kuna ni kweli mbingu ipo! Usistaajabu Yesu Kristo alipokuwa hapa duniani Aliwaonya watu kuhusu kuzimu. Nasema tena, kuzimu ni halisi. Niliiona na ni mahali pa kutisha. Nikamwuliza : " Ni nini ?" Jibu lake lilikuwa : "**Hii imetayarishwa kwa ajili ya shetani na malaika wake na kwa walioasi**" Akataja kwa majina yao kama ilivyoandikwa katika Ufunuo 21:8: "Bali waoga na wasioamini na haramu, na wauaji, na wazinzi na wachawi, waabudu sanamu na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti ambayo ni mauti ya pili " .

Tulipoenda katika chumba tano na Alipofungua pazia, nilichoona kinaweza tu kuelezewa kama UTUKUFU. Ilikuwa ni kama tunangalia kutokea kwa juu. Niliona **mji mpya**. Mji ulikuwa ni mkubwa na mzuri! Mitaa ni ya dhahabu. Majengo hayawezi kulinganishwa na kitu chochote katika dunia hii. Alisema: " **hili ni tumaini la watu wa Mungu**. Je, utakuwepo mahali pale "Haraka nikajibu" Ndiyo " Baada ya hayo tulirudi katika kiti cha enzi na Akasema: "**!Nenda kashuhudie nini nilichokufanya** "

Tena, alinichukua mpaka katika chumba kingine na alipofungua pazia nikaona mambo yote ambayo nilikuwa naenda kukutana nayo kwenye safari yangu ya kwenda Onitsha na Lagos na jinsi gani hatimaye atanikombua. Baada ya hayo Akaniambia : "**Usiogope, nenda, nami nitakuwa pamoja nawe.**" Aliniongoza, nje ya ukumbi na akatoweka kabisa, na mara nikaamka kwenye kitanda katika nyumba ya mwanaume mwengine. Nikapiga kelele, mtu na mke wake wakakimbia kutoka katika chumba chao. Wakachungulia na kisha wakaingia "Kwa nini niko hapa? " Niliuliza. Mwanaume yule ndio alielezea jinsi nilivyoanguka katika teksi na jinsi walivyonipeleka kwenye kanisa la Katoliki pale Owerri. Jinsi walivyomleta Daktari, ambaye alikuja na baada ya kunichunguza afya yangu alisema mapigo yangu yalikuwa ya kawaida na kwamba wanapaswa kusubiri na kuona nini kitatokea. Daktari akawapa uhakika kwamba nitapata nguvu tena. Ndipo alinichukua kwenye gari lake mpaka nyumbani kwake na alikuwa akisubiri. Pia alikiri kwamba hakujuwa kwa nini alimuamini Daktari na kwa nini alichukua jukumu la kunichukua mpaka nyumbani kwake.

Waliniuliza jina langu na anwani ambayo niliwapa na baada ya hapo niliamua kukaa kimya na sikuwaambia uzoefu wangu huo. Nilikaaa kwa utulivu na familia hii yenye wema kwa siku mbili na kisha mtu huyu na mkewe walinipeleka mpaka kituo cha magari cha Owerri, ambapo nilichukua teksi na kwenda Onitsha. Yote yale Bwana alinionyesha kuhusu safari yangu yalitokea moja baada ya jingine. Nilichukua teksi nyingine ya kwenda Lagos. Jambo la kwanza asubuhi iliyofuata. Nilitii na kuondoka Lagos kuelekea Port Harcourt. Huwa najiuliza mara nyingi, kwa nini Bwana aliamua kuniokoa mtu kama mimi. Mtu muovu na muharibifu, wakala wa Shetani ! Nilipata jibu katika maneno haya matatu: **Mungu ni upendo**. Hakika, Mungu ni Upendo! (1 Yohana 4:8 , 4:16)

Sura6: Vishawishi na Ushindi

« Kondoo wangu huisikia sauti yangu; mimi nawajua, nao hunifuata. Mimi nawapa uzima wa milele; nao hawatapotea milele, wala hakuna mtu atakayeweza kuwatoa mkononi mwangu.» Yohana10: 27-28

Baada ya kubadilika na kwenda kwa Kristo, jambo la kwanza lililotokea ni kwamba zawadi zote kutoka baharini, darubini, TV, mashati, picha nilizopiga nikiwa ndani ya maabara za baharini na picha ya Malkia wa Pwani ambazo zilionekana katika gorofa yangu zilitoweka.

Niliporudi Port Harcourt, nilikuwa na hamu ya kushuhudia kile Bwana alichonifanyia kwa ajili yangu lakini sikuruhusiwa ndani ya kanisa . Mke wa marehemu mjomba wangu, ambaye pia ni Mkristo, alinichukua mpaka kwa mchungaji mmoja, lakini swali alilouliza ilikuwa ni: "Je, ameleta karatasi?" Ilikuwa ni baadaye sana nilielewa kwamba karatasi ilikuwa ni 'barua ya uanachama. Barua ya uanachama inahusika vipi na ushuhuda wangu wa nguvu ya Kristo na kile amefanya kwa ajili yangu- Mungu, amenikomboa kutoka katika nguvu za giza na kuniingiza katika ufalme wa Mwana wake mpendwa, ambaye nimepata ukombozi kupitia damu yake, yaani, na hata msamaha wa dhambi zangu ?

Nilihuzunika, baada ya kujua kwamba Shetani haruhusu waumini wachanga kwenda na kushuhudia, hasa wale ambao hapo awali walikuwa washiriki wakubwa katika shughuli zake , na anafanya kila kitu kuzuia shuhuda hizo. Tena nikakumbuka, ni dhahiri Bwana aliniagiza "**kwenda na kushuhudia kile amenifanyia**" na hapa nilikutana na kipingamizi. Labda ilikuwa bado si wakati wake. Hivyo niliamua kuachana na kutoa ushuhuda wangu kwa mtu yejote. Nilisafiri na wafanyabiashara watatu kutoka Aba kwenda Togo kwa safari ya kibiashara. Pale nilinunua bidhaa yenye thamani ya N160,000 (Mia moja na sitini elfu za Naira). Kati ya pesa hizi pesa yangu binafsi ilikuwa ni shs N70,000 na nyine yote iliyobakia N90 ,000 nilikopa kwa wafanyabiashara wa Aba. Miiongoni mwa mambo niliyonunua ilikuwa ni furushi la kamba, madawa mbalimbali (hasa antibiotics) , sindano, vipimajoto, nk

Nilipofika mpakani mwa Nigeria, Tulishikiliwa kwa ajili ya ushuru wa Forodha na baadaye tulitakiwa kutoa rushwa. Tulikataa na bidhaa zilikamatwa ikiwa ni pamoja na zile za wenzangu. Miezi michache baadaye, Ile mizigo ya wenzangu ilitolewa, ila yangu haikuruhusiwa. nilirudi baadaye na nikaambiwa kulipa N40,000, lakini nilipoangalia mali yangu ile niligundua kwamba bidhaa zote muhimu, kama furushi la kamba, sindano, madawa, nk, tayari vilikuwa vimeibiwa. Nilitathmini bidhaa iliyobaki na nikajua kwamba kulipa N40,000 kwa ushuru itakuwa tu ni kuongeza hasara, hivyo niliamua kuachilia bidhaa iliyobaki.

Wafanyabiashara ambao niliwakopa fedha walianza kunifukuzia. Baadhi waliwaita polisi, wengine walichukua sheria mkononi mwao na wakapanga kunifanyia kitu kwa maisha yangu. Suluhihi pekee ilikuwa ni kufunga akaunti yangu Bank na kutumia fedha zote nilizokuwa nazo kulipa madeni yote. Kwa neema ya Mungu, nililipa yote isipokuwa N1,000 ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya mwenye nyumba wangu Lagos. Nilikuwa mufilisi kabisa na nilikopa hata 20k kwa ajili ya nauli ya teksi.

Nilikwenda kwa wakristo wachache niliowajua, ili kutafuta msaada wa kuniwezesha kuanza upya. Hakuna aliyesema ndiyo au hapana, badala yake waliniishi niende siku inayofuata kila mara nikachoka kwa habari ya kutafuta msaada. Sikujuu neno la Mungu pamoja na kuchanganyikiwa katika moyo wangu nilisoma Biblia bila kuelewa. Wakati bado natafakari nini cha kufanya, nilipokea simu ya haraka kutoka kijijini mwangu. Nilikimbia nyumbani na kukuta kwamba jengo dogo nililokuwa nimeanza kujenga liliikuwa limevunjwa na mjomba wangu ambaye pia alikuwa ametishia kuniua. Asili yangu ya kale ndani yangu ilishtuliwa. Nikakumbuka wakati nikiwa na jamii ile ya baharini (secret society), jinsi alivyokuwa akinilogopa na alikuja kwa magoti mbele yangu. Lakini sasa alijuu nimebadilika (jinsi alivyojua sikujuu kwani sikuwa nimesafiri kwenda nyumbani tangu nilipobadilika)

na sasa alinitishia. Nilimuita Bwana na nikasema: "Basi, wewe umeniokoa mimi na kuniacha nimevurugika na kuruhusu adui zangu kufurahia juu yangu! " Nililia kwa sauti nikadhamiria kurudi kwenye ile jamii ya kichawi.

Angalau wanaweza kuniokoa kutoka katika kuchanganyikiwa kote huku na pia watafundisha mjomba wangu somo ambalo hatasahau maisha yake yote. Ingawa nilifanya uamuzi huu, nilikuwa na hofu mbili ndani yangu

1. Wakati nilipokuwa nabadilika, Bwana aliniweka wazi akaniambia: "**Hii ni nafasi yako ya mwisho.**" Ukrejea tena kwenye jamii ile ina maana ni kifo, sio tu kifo cha kimwili lakini pia cha kiroho.

2. Kama nikibakia katika Bwana, mjomba wangu alikuwa anatishia kuniua.

Nilichanganyikiwa na nilihitaji msaada. Nilikuwa mjinga wa neno la Mungu na kamwe sikujua kile ambacho Neno linasema kwa habari ya hayo juu. Ndugu msomaji , utagundua hapa kwamba nilikuwa na mchanganyo huu wote kwa sababu ya ukosefu wa mfuutiliaji nikiwa bado mchanga. Kuwafuatilia waongofu wachanga ni muhimu sana na Wakristo wanapaswa kuchukulia hili kwa umakini. Kama unajua huwezi kufuatilia muumini mchanga, tafadhalii usiende kushuhudia. Yesu Kristo alisisitiza hili mara tatu Alipomuuliza Peter: " Simoni, mwana wa Yona, wanipenda mimi zaidi kuliko hawa? ... Lisha kondoo wangu. "Wengi wa waongofu wapya wanarudi nyuma kwa sababu ya kukosa ufutiliaji mzuri. Kama unampenda Yesu, jali kondoo wake!

Vita na shetani

Katika kipindi hiki mawakala wa Malkia wa Pwani walianza kunitafuta sana. Niliteseka sana katika mikono yao. Nilikuwa na ndoto mbaya. 1 Mei 1985, mwezi mmoja baada ya kuokoka saa 02:00 usiku, wengine katika nyumba walikuwa wamelala. Niliamshwa na mawakala hawa. Wakaniamuru kutoka nje ya nyumba. Nilitii, nikatoka nje na walinifuata nyuma. Ilikuwa kama yote yanayotokea ni ndoto, lakini hii ilikuwa katika uhalisia. Tulitembea mpaka juu ya ardhi ya maziko kanisa la Mtakatifu Paulo Anglican , off Aba Road, Port Harcourt.

Tulipofika pale walisema: "Ni lazima urudi. Kama ukikataa tutakuua au kukufanya fukara. "Baada ya maelekezo haya waliondoka. Nikapata ufahamu wangu na kujishangaa nimefika vipi pale makaburini. Nikarudi kitandani na kulala. Waliamua kuwa wananihambulia mchana. Mara kwa mara, wakati natembea kandokando ya barabara walijaribu kupambana na mimi. Wengine karibu yangu waliniona napambana na hewa au kuniona nakimbia kama mtu anayefukuzwa.

Mimi peke yangu ndiye niliewaona. Basi, walifanya hivyo kwa mara nne na wakaacha. Kisha kiongozi wao , Malkia wa Pwani, achukua jukumu. Siku ya kwanza alikuja katika gari ambalo aliliegesha kando ya nyumba yetu. Alikuwa amevaa vizuri na kama kawaida yeye ni mzuri sana. Watu walionzunguka walimchukulia kuwa ni mpenzi wangu. Mara akaingia ndani nilijua alikuwa ni nani. Alikuja saa 12.00 mchana wakati eneo lote lilikuwa busy kidogo. Akakaa chini na mionganini mwa mambo mengine aliyoysesema ni: " Unaweza kwenda kanisani kwako, amini chochote unachotaka kuamini, **lakini kama tu hautanitangaza**, nami nitakupa chochote kile katika maisha haya " Sikuwa nimejua maandiko hivyo nilimsikiliza na kumuangalia anatembea tembea pale. Aliomba na alijaribu kunishawishi nirudi kwake. Sikusema ndiyo au hapana kwake. Alisimama, akaenda ndani ya gari yake na akaondoka.

Kama mara mbili hivi mke wa mjomba wangu alimkaribisha nyumbani kwake bila kujua alikuwa ni nani nami kamwe sikuwahi kumwambia mke wa mjomba wangu alikuwa ni nani. Ziara yake ya mwisho alibadili namna yake ya kunisihi. Wakati huu alinipa onyo kali akisema kwamba amejaribu sana kunibembeleza nirudi kwake na kwamba nimekuwa mkaidi sana, na kwamba hii ilikuwa ni ziara yake ya mwisho. Kama bado nakataa kurudi, atakuja mwezi Agosti ama kuniua , au kunilemaza au kunifanya maskini. Kisha akaondoka.

Nilikuwa na hofu, hivyo siku moja nilikwenda kanisani na kumuita ndugu mpendwa. Nilimwambia matatizo yangu na mtazamo wangu juu ya baadhi ya washirika wa kanisa , nk Huyu ndugu alinipa anuani ya ofisi ya umoja

wa maandiko (Scripture Unions) na akaniambia: " **Pale watanipatia msaada**" Siku hiyo ilikuwa ni siku ya mwisho kumuona huyu " ndugu." Sijawahi kumuona popote Port Harcourt mpaka leo. Nilichukua anwani na siku iliyofuata, nilichukua teksi mpaka No 108 Bonny Street, ambapo zilikuwa ofisi hizo ni na kukutana na mchapaji ambaye alinipa robo ya mpangilio wa shughuli za Umoja wa Maandiko (SU) Kundi la Rumuomasi Pilgrims, wakiwa ndio karibu na mimi. Akasema: " Njoo siku ya Jumapili! " Nilikuwa pale katika Fellowship Centre - Shule ya St Michael's State , Rumuomasi - saa 8:00 mchana, bila kujua kwamba ibada inaanza saa 9:00 mchana, lakini nilikutana na kikundi cha maombi, hivyo nikajiunga nao .

Baada ya ibada siku hiyo nilijua kwamba mahali pale palikuwa sahihi kwangu.Mungu akanipa msichana ambaye alikuwa kama mama kwangu, ye ye alijitoa kikamilifu katika kunielezea Neno la Mungu na kunishauri pia. Ndugu wakaonyesha utayari na kunijali. Niliona Upendo wa kweli. Roho Mtakatifu alianza kunipa ufahamu wa Neno la Mungu na imani yangu ilikua. Lakini Malkia wa Pwani hakujionyesha kwa sababu aliwekwa wazi. Zaburi 91, Ulinzi wa Mungu, ultimia katika maisha yangu. *Isaya 54:17: "Silaha yoyote itakayofanywa juu yako haitafanikiwa, na ulimi wowote utakaoinuka juu yako katika hukumu wewe utauhukumu. Hilo ndilo fungu la urithi la watumishi wa Yehova, na uadilifu wao ni kutoka kwangu,"* asema Yehova.. "Hii pia ilitimia.

Septemba 1985, Nilipokea ujumbe kuwa jina langu limeonekana kama msambazaji wa Silver Brand Cement, Lagos na kwamba nilitakiwa kufika ofisini tarehe 27/9/85.Nilliondoka Port Harcourt tarehe 26/9/85 na kufika Lagos usiku. Asubuhi iliyofuata 27/9/85, nilikwenda ofisini nikaambiwa na Meneja Utumishi kuwa sehemu yangu ilijazwa na mtu mwengine. Akanieleza nifike siku iliyofuata tarehe 28/9/85 kumuona Mkurugenzi Mtendaji. Nilipokuwa njiani kuelekea nyumbani kwangu, nikipita njiani, mtu akaja kutoka nyuma na kunikaba na akajaribu kubana pumzi yangu na mdomo wangu kwa pamoja. Nilijitahidi kuokoa maisha yangu, na ingawa watu walikuwa wanapita, hakuna aliyejuja kuniokoa, lakini Bwana aliingilia kati. Wakati mimi bado najitahidi kwa mikono nikasikia akilia kwa sauti na kenisukuma mbali akisema : "Ni nani huyo aliyeo nyuma yako? " Alirudia mara ya pili na kutoweka. Kutoka kwa sauti nilijua alikuwa ni mwanamke lakini kamwe sikumuona ni nani. Nilichanganyikiwa na kupigwa na bumbuwazi.

Hapa tena mwenye nyumba wangu alikuwa na hasira sana na akasema: " Kwa nini umekimbia na fedha ya kodi yangu?" Nilimsihi na nikajaribu kumuelezea kwamba kwa sasa mimi si kazi na nitamlipa fedha zake zote kwa haraka mara nipatapo fedha.

Kwa jinsi alivyoonyesha nilifikiri suala hili limeisha. Siku iliyofuata 28/9/85, nilikwenda na kukutana na Mkurugenzi mtendaji ambaye aliomba msamaha kwa kumpa nafasi yangu mtu mwengine. Alipokuwa bado anaongea kijana mmoja akaingia na kuniuliza: " Je, wewe sie Emmanuel? "Nikasema ndiyo ni mimi: "Ndiyo , mimi niko. " Akasema: "Ndiyo, hatimaye tumekupata sasa! Je, umemaliza kukimbia? Tumetembelea mara kwa mara Port Harcourt na kugundua kwamba daima huwa unatembea na mama yako wa kiroho. Amekuwa kikwazo sana kwetu na sasa kwa sababu umekuja Lagos tumekukamata! Hautarudi tena Port Harcourt. Mimi ndiye nimechukua nafasi yako " Nikampa changamoto na kumwambia : " Huwezi kunifanya kitu chochote " Mkurugenzi Mtendaji alishangazwa na kile kilichotokea katika ofisi yake ! Nikaomba radhi mwenyewe na nikarudi nyumbani.

Dakika chache baadaye nikasikia mlango unabishwa na NINA akaingia. Akaniuliza kama nilikuwa narejea Port Harcourt. Nikajibu ndiyo. Aliniomba nirudi kwao akanieleza kuwa kazi nilizokuwa nimefundishwa zilikuwa hazipatikana mtu wa kuzirithi: KOTIPARI (katika lugha ya Kiyoruba). Nilikuwa nimepatiwa mafunzo :

- Kuwa juu ya mawakala wa nguvu za mapepo.
- Kuwa juu ya " chumba cha bahari cha maelekezo, " kufuatilia matukio katika dunia, kutuma na kupokea ishara, na kuhamasisha majeshi, nk
- Kuwa karibu na Malkia wa Pwani. Hii inahusisha si tu sherehe, sadaka , utekelezaji wa kazi maalum

alizonitura, lakini pia mambo mengine magumu kuelezea.

- Kwa msaada wa nguvu za giza , kuanzisha jamii mpya za siri(jamii ya kichawi) ambazo zitaonekana hazina madhara ili kuwavutia vijana na zaidi waendaji tu wa kanisani .

Alisema, kama ataongozana naye, kilichokuwa kinanisubiri ni mara mbili ya baraka za kwanza. Alikiri kwamba walihusika kwa mali yangu kukamatwa na kuibiwa, pia kwamba wao ndio waliomchochea mjomba wangu kuharibu jengo langu na kutishia maisha yangu. Kwamba kama nikikataa kumfuata, wangefanya zaidi na kuhakikisha kwamba sitafanikiwa. Kwamba walikuwa wameamua kupambana mama yangu wa kiroho: "Kama tutampata ye, tumekupata wewe" alisema. Wakati huo, Nilianza kumhubiria. akasimama na kusema: "Wanakudanganya, " Akaondoka. Hii ilifanyika jioni ya tarehe 28/9/85 .

Mara dakika tano zikapita nikasikia mwingine anabisha. Wakati huu walikuwa watu wanne. Wakanionyesha ishara nitoke nje na nikajiona mwenyewe naanza kuwafuata. Tulitembea hadi katika nguzo 2 na mmoja wao akaniuliza: "Je, unatujua sisi? " nikasema hapana. Aliendelea kusema: " Tumeajiriwa na mwenye nyumba wako tukue." Wakati anaendelea kuzungumza mmoja wao akatoa bunduki na mmoja akatoa sime. Sikujua cha kufanya, nilijua kuwa wataniua, lakini Mungu katika Njia zake za ajabu akafanya ishara ambayo ilinishangaza mimi na wenyewe.

Mtu aliyekuwa na bunduki akanifyatulia risasi lakini hakukuwa na sauti. Mtu mwenye kisu akakitumia nyuma ya mgongo wangu lakini hakuingia ila tu kililia kama mtu anamchapa fimbo mtu. Walikuwa na hofu kama mimi. Roho wa Mungu alikuja juu yangu na nikaanza kuhubiri. Watatu wao wakakimbia, lakini mtu wa nne akaanguka na akaanza kulia na kuniomba nimuombee. Sikuweza hata kujua nini cha kuomba wakati huo lakini nilisema tu: " Bwana, tafadhali msamehe, Msamehe bwana. Amina! " Aliyalitoa maisha yake kwa Kristo, Nilimpeleka kwenye kanisa la Pentekoste na alielezea kile kilichotokea kwa Mchungaji. Nilimkabidhi kwa Mchungaji na nikaondoka. Nilipoingia tu ndani ya nyumba mwenye nyumba akaja anakimbia na akapiga magoti akinisihi: " Tafadhali nisamehe. Nilidhani uliamua kukimbia kwenda Port Harcourt kwa sababu ya fedha yangu (N1,000). "Nilimsamehe na hatimaye tulikubaliana kwamba fedha ilipwe kwa awamu .

Usiku huo, mida ya saa 08:00 usiku Bwana aliniamsha. Sikuweza kujua kwa nini niliaamka nikaenda sebuleni na nilichokiona ilikuwa ni kobe mkubwa ananifuata. Mara nikakumbuka shule ya kujifunza Biblia tulipokuwa Port Harcourt, juu ya nguvu katika neno. Ndipo nikasema maneno haya: " Kobe , tangu nilipozaliwa , nyumba ya kobe ni ama kichakani au baharini, lakini kwa kuja ndani ya nyumba wakati madirisha na milango ni imefungwa umefanya dhambi, na kwa sababu hii ni lazima ufe. "Mara baada ya kusema hivi akatoweka kabisa. Nilikwenda chumbani na kulala. Mara ya pili tena, niliamka na kusikia kelele sebuleni. Nilikwenda na tazama mbele yangu ilikuwa ni kitu cha kutisha. Nikarudia maneno yaleyale na mara baada ya kusema: "Kwa kutenda dhambi hii lazima kufa, " kikatoweka pia. **Wakati wa safari hii ya Lagos niliona wema, ukuu wa Mungu na uaminifu wake.**

Asubuhi iliyofuata tarehe 29/9/85, nilichukua basi zuri sana mpaka Port Harcourt. Nilipofika Ore ,basi likagonga mti. Liliharibika kidogo lakini hakuna mtu aliyejeruhiwa. Dereva akalivuta kwenye barabara na akaendelea kuendesha, basi likaanza kuyumba kutoka upande mmoja wa barabara hadi mwingine. Nikakumbuka vitisho nya NINA, hivyo nikasimama katika basi, na kuhubiri nilihitimisha kwa kusema : "Ni kwa sababu yangu mimi haya yanayotokea. Lakini tangu sasa , hakutakuwa na ajali mpaka tufike Port Harcourt, katika jina la Yesu ! "Na mimi nikakaa. Kwa kweli, wakati nimeketi nilishangaa, kitu gani nimekisema. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Gari lilitembea vizuri mpaka Port Harcourt. Hakukuwa na ajali zaidi au kuharibika. Biblia inasema sawa kuwa;"*Mtu yeyote akishambulia, haitakuwa kwa maagizo yangu.Yeyote atakayekushambulia ataanguka kwa sababu yako.*"(Isaya 54: 15). Wao (Malkia wa Pwani na mawakala wake) walijaribu, lakini kwa sababu mkutano wao haukuwa katika Bwana bali kinyume na mtoto wake ,wote wakajikwaa na kuanguka. "Pindi adui atakapokuja kama mafuriko ya mto, Roho wa Mungu atainua kiwango dhidi yake" (Isaya 59: 19). Nampa Mungu utukufu wote kwa ajili ya kujionyesha mwenye nguvu kwa niaba yangu.

Sura7: Shughuli za mawakala wa shetani

« Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. »
Waefeso. 6: 11-12

Kitabu hiki hakitakuwa kamili kama mbinu mbalimbali za uendeshaji wa mamlaka hizi hazitawekwa wazi. Pia ni muhimu kwamba aina mbalimbali ya namna na jinsi zinavyojitokeza ziwekwe wazi.

Jambo moja li wazi nalo ni kwamba ni shetani atakuchochea uamini kwamba yeche ni hadithi tu za kufikirika au mawazo ya uovu ambayo ni rahisi, au atakufanya uone zaidi sana kwa habari ya nguvu zake na mamlaka ya Mungu iwepo chini. Biblia inasema: " *Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.* Biblia inasema kwamba silaha za Wakristo dhidi ya shetani na mawakala wake " *si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome, tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiiinuacho juu ya elimu ya Mungu , na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo*" (2 Wakorintho 10: 4-5). Tena maandiko yanasema: wazi " *Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhahirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi*" (1 Yohana 3: 8). Yesu baada ya kuzivua enzi na mamlaka, alifanya onyesho la waziwazi, alishinda dhidi yao .

"*Basi umetegwa kwa maneno ya kinywa chako, Umekamatwa kwa maneno ya kinywa chako,*" (Mithali 6:2). Hivyo mtoto wa Mungu ni lazima kuwa makini kukiri neno la Mungu, ambalo Mungu ameahidi ataharakisha kulifanya. Kuna ukiri mara tatu umesemwa katika neno la Mungu

1. Ungamo la Uongozi wa Kristo.
2. Ungamo la imani katika Neno, katika Kristo na katika Mungu Baba.
3. Kukiri dhambi.

Tunaposikia neno "kukiri , " sisi kwa urahisi tunafikiria kwa habari ya dhambi. Kamusi inafafanua kukiri ni :

1. Kuanzisha kile kitu tunaamini.
2. Kushuhudia kwa kitu ambacho tunakijua.
3. Kushuhudia ukweli ambao tumeridhia .

Kwa hiyo inapaswa kusikitikiwa kuwa tunapotumia neno kukiri (confession) kwenye fikra zetu tunafikiria dhambi. Mwandishi yuko hapa kukutia moyo mtoto wa Mungu kuanza leo kukiri kile Mungu amesema. hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema na akatufanya tukae katika mbingu (juu sana zaidi ya enzi na mamlaka) katika Yesu kristo. Kwa hiyo Wakristo wanapaswa kutambua ambapo wamekaa. Wanapaswa kujua kwamba wanatembea katika urefu huo, juu ya Shetani na mawakala wake. Bwana Yesu Kristo amewapa ninyi nguvu zote na mamlaka ili kwa hizo tupate kuwa washirika wa uzima na utauwa (2 Petro 1 : 3).

Mungu hakuwa na kusudi la kwamba mazingira yawatawale watoto wake, badala yake neno la Mungu katika kinywa cha Mkristo ni lazima kidhibiti hali/mazingira yake. Mungu alisema katikaYer. 23:29 akisema: "Je, si neno langu kama moto? asema Bwana, na kama nyundo ivunjayo mawe vipande vipande?" Wakristo, Namaanisha waliozaliwa mara ya pili, wanapaswa kutambua kuwa wakati jina la Yesu linatamkwa, kile kinachotoka nje ya vinywa vyao ni moto. Mkristo anaposimama juu ya mamlaka aliyopewa na Kristo na anatoa amri kwa jina la Yesu, moto hutoka katika kinywa chake na pepo lolote kudhibiti hali husika ni lazima kutii. Yesu yu hai leo ili kuangalia kwamba kila neno lake linakuja kupita. Tena, nataka kuonyesha ukweli muhimu kuwa

Wakristo wengi wanatazama kijuu juu , na hiki ndicho ambacho Shetani anatumia. Yesu, baada ya Peter kumsema kwake kwa habari ya ule mtini uliokauka baada ya kulaaniwa na Bwana , alisema:

(Matthew's account) “*Amin, nawaambia Mkiwa na imani, msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima huu, Ng'oka, ukatupwe baharini, litatendeka. Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.* (Matt. 21: 21-22).

(Mark's account) “*Mwaminini Mungu. Amin, nawaambia, Ye yote atakayeumbia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.* (Marko 11: 22-23).

Hapa Yesu anaonyesha mamlaka ya neno lilitotamkwa na linahamasisha Mkristo awe na mlengo sahihi katika maombi yake na katika kutumia mamlaka yake. Baadhi ya wakristo wanaamrisha milima ihame lakini hawaambii milima hiyo iende wapi. Yesu alisema kama ukiuambia mlima huu **ng'oka na akajitupe baharini**...Ngoja tuchukue hiki kisa cha kukemea pepo kwa mfano. Baadhi ya wakristo wanakemea na kufukiza pepo bila kuwaambia waende wapi sehemu maalum. Ni hatari. Ukishafunga pepo kweli linafungika. kama ukikemea bila kulipeleka sehemu maalum, linabaki linazungukazunguka tu maeneo maeneo. Kama pepo akikemewa tu kutoka nje ya mtu anaweza kurudi baadae au kuingia kwa mtu mwingine yejote wa maeneo hayo ambaye si Mkristo. Kwa hiyo Mkristo anatakiwa awe makini anapokuwa anahuksika na mapepo. Hakikisha pepo amefungwa, kutupwa na kufukuzwa kwenda sehemu husika (*na kuzuiliwa kurudi tena*)

Baadhi ya wakristo wakati wanaomba husema : "Nawaweka chini ya ulinzi mapepo katika jina la Yesu. " Katika ulimwengu wa roho kweli unaona mapepo amesimama wima yanashirika kwa amri ijayo. Lakini kama Mkristo atayaacha katika hatua hiyo, basi hajamsaidia mwathirika. Usimchezee chezee shetani. Hutakiwi kucheza na adui yako. Mungu amekutuma wewe kwenye huduma ya ukombozi na maridhiano (kupatanisha watu kwa Mungu). Kwa hiyo ni lazima kuwa makini kufanya kazi ya uhakika. Narudia, unnamfunga pepo, anafungika. ukimtupa mahali popote inakuwa hivyo. Lakini pale utakapoamua kutoishi katika dhambi lakini kwa mapenzi ya Mungu, chochote kuhusu amri unapokitoa kwa shetani au mawakala wake katika jina la Yesu lazima watii. Mungu ameahidi kutimiza kila neno la lake. Tunapokwenda katika hatua nyingine , Udhahirisho wa nguvu za shetani na mawakala wake, ningependa uwe na mistari hii katika fikra zako:

1. "Ninyi ni kamili katika Yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka" (Kol. 2: 10).
2. "Sasa, mimi nawapeni nguvu (mamlaka) wa kukanyaga nyoka na ng` e, na uwezo juu ya nguvu zote za yule adui , wala hakuna kitu chochote kitakachowadhuru ninyi . " (Luka 10:19)
3. " Tazama, watakusanyika pamoja lakini si kwa sababu yangu. Mtu yeyote atakayekusanyika dhidi yako ataanguka kwa ajili yako. Hakuna silaha itakayofanyika dhidi yako itafanikiwa : na kila ulimi utakaoinku kinyume chako ili kukuhukumu basi wewe utauhukumu, Huu ni urithi wa watumishi wa Bwana, na haki zao ni mimi. "

Nataka kuonyesha katika kitabu hiki kuwa hizi nguvu za giza zinafanya kazi katika kanisa, masoko, maeneo ya makaburi, misitu, hoteli,baharini na angani.

Ndani ya Makanisa

Sisi ni mashahidi hivi leo kuna watu wengi wanapepo kanisani. Baadhi wananaena katika lugha na hata wengine wanatoa unabii.Ni wale tu walio na Roho wa Mungu ndio wanaoweza kutambua hawa wenzetu. Lakini tuko hapa kujadili mawakala wa shetani katika kanisa. Tena hatujadili wanachama wa siri wa ibada za kijadi/kichawi ambao wako kanisani(baadhi yao ni viongozi) Tunafahamu wako pale. **Ninao waongelea ni wale walio kuja kama mawakala wa shetani:**

1. Kusababisha vurugu na machafuko kanisani.
2. Kutawanya washirika.
3. Kuwafanya wanaume na wanawake walale pindi neno linaendelea.
4. Kusababisha uharibifu wa namna mbalimbali wakati ibada inaendelea.
5. Kuvuna roho kwa ajili ya shetani.

Kwa kuwa nimekwisha kusema mabo machache hapo juu katika sura ya tatu, Nitakupa ushahidi wa kile kilichotokea katika siku za karibuni. Wakristo wanapaswa kukaa na kila neno la Bwana Yesu Kristo, kwa sababu wakati waapoasi au wanapokuwa wanajirizisha basi wanakabiliwa na hatari ya kuanguka katika vishawishi nya Shetani au mawakala wake. Wakristo wameitwa kutoka katika giza na kuingia katika mwanga wa Mungu. Wakristo wameitwa kujitenga mbali na dunia na chochote inachokitoa. "**Tokeni kati yao na mkatengwe,**" (2 Kor. 6:17) yanasema maandiko.

Kulikuwa na dada huyu, dada J (jina limehifadhiwa). Yeye alikuwa amezaliwa tena na alikuwa mwanachama kamili wa moja ya makanisa hai. Baadaye aliamishia ushirika wake na kuja kwenye ushirika wangu. Alifanya shughuli zote za kanisa na alikuwa mchapakazi kwao. Lakini tabia yake hatua kwa hatua ikawa ni ya mashaka. Hivyo wachache wetu tuliamua kumtembelea katika nyumba yake ili kujua nini kilikuwa ni tatizo. Wakati tunamhoji, roho chafu ndani yake zilikasirika zikaanza kujidhihirisha, na zikasema kuwa alikuwa ni wakala wao pale kanisani. Mapepo hawa walitolewa nje yake na ukombozi ukafanyika ndani yake. "Dada, imekuwaje mpaka unakuwa wakala wa Shetani, lakini pia ni muumini mzuri wa kanisa?" TulimuulizaAlichotuambia ni hiki kifuatacho: Ilianza siku moja, baada ya ibada ya Jumapili, 'dada mmoja'(muumini wa kike katika Kristo, kama alivyodhani) alikuja kwake na alionyesha hamu kubwa ya kuwa karibu yake kwa sababu, kwa mujibu wa huyu 'dada huyo' alivutiwa na maisha ya dada J ya Kikristo. Alikubali urafiki wake bila kujihoji. Wote wawili wakaenda nyumbani kwake dada J na anayejiita 'dada' akaleta ndizi na karanga, ambazo wote wawili walikuwa wakila. Alikaa kwa Sister J kwa muda na baadaye akaondoka.

Ziara zake zikawa mara kwa mara, na katika kila ziara aliletu zawadi kwa dada J. Zawadi zilikuwa tofauti kama vile nguo, viatu, fedha, nk kwenye baadhi ya tafrija huyu dada alikuwa anakuja na wasichana wengine wengi. Aliendelea kufanya hivyo kwa kipindi na wakati 'dada' huyu alipoona kwamba amefanikiwa kuuondoa mwanga wa Kristo. Alibadilika na akaanza kumtembelea Sister J katika roho. Dada J kisha akapewa nguo nyekundu, jiwe la baharini, pete kwenye kidole gumba chake cha kulia mguuni, na mkufu wa kuva kwenye kifundo cha mguu wake. Kwa sababu alikula vitu vyao vingi na alikuwa amechukua vingi kutoka kwao, hakukuwa na namna ya kugeuka. Aliingia mkataba pamoja nao na akaanza kuhudhuria vikao vyao. Aliweza kujibadili kuwa nyoka, popo nk. Kisha baadae akawa wakala wao kuvuna roho kwa ajili yao katika kanisa.

Sifa ni kwa Mungu yeye hivi sasa amekombolewa! Zawadi zote tulizompa ziliharibiwa na sasa ni mwenye furaha tena katika Bwana. Ndugu msomaji, Hii ilianza na urafiki usiokuwa wa kawaida, na kwa sababu Sister J alikosa roho ya utambuzi na wala hakuwa na macho kama alivyoamriwa na Bwana "**Kesheni na muombe msije mkaingia majaribuni,**" (Marko 14:38) alipotea na akaanguka katika kina kwenye mikono ya adui na mbio zake zingeweza kuishia kuzimu kwa sababu ya uzembe. Unaweza kwa urahisi kutambua mawakala wa Shetani kwa vitu vifuatavyo:

- Wanavaa pete kwenye moja ya vidole vikubwa, mkufu kwenye mguu, pete za puan , bangili zisizo za kawaida mikononi, nk
- Wanaweza kuingia hata kanisani au kwenye vikundi nya ibada na kuwa na bidii sana katika shughuli za kikundi au kanisa, kwa ajili ya Mkristo mmoja wanaemtafuta. Baadhi wanaishi katika tabia isiyo ya kawaida , wengine ni waovu, nk.

Hii ndiyo maana mtoto wa Mungu anatakiwa amwombe Mungu kwa roho ya utambuzi wa roho, ili kumwezesha kuzitambua mara moja. Pindi wakijua umewatambua, wanahakikisha hawaji karibu na wewe. Sababu ikiwa ni kwamba kiongozi wao anawaonya juu yako!

Maeneo ya soko

Wanafanya kazi kwa namna mbalimbali katika soko. Soko ni moja ya maeneo yao makubwa ya shughuli, kama vile hotelini ni mahali ambapo wao hukaa kusubiri wanaume. Katika soko, wanachukua wahanga wao, baadhi ya wanawake wajawazito ambao mimba zao huaribika husababishwa na wao ili kuwawezesha kupata damu kwa ajili ya benki yao ya damu. Baadhi ya waathirika wanaweza kuongozana nao ili wawatembelee usiku. Hii hutokea kwa wasioamini ! Baadhi ya bidhaa huuzwa katika soko mfano shanga, lipsticks , ubani, na vitu ya chakula kama vile dagaa "Malkia wa Pwani" nk,vinachimbuko lake huko.

Kuna matendo fulani Wakristo wanapaswa kuangalia, kwani unaweza kuona mwanamke au labda kijana ambaye ghafla kakugusa tumboni au sehemu yoyote ya mwili wako. na inasababisha ugonjwa. Mkristo kwa hiyo ni lazima, anapopitia hili, kutoa neno la amri katika jina la Yesu, akitawanya au kuharibu mipango ya shetani , nk Na uhakika wa kutosha ni kuwa chochote unachotawanya au kufunga hapa duniani itakuwa hivyo. (Mathayo 16:19, Mathayo 18:18)

Shughuli za Kijadi

Pia ni muhimu sana kutambua kwamba watu wengi wanaingizwa katika shughuli za Shetani au kupata mapepo kupitia kwa zaidi kwenye sherehe hizi za utamaduni na ngoma. Ngoma nyingi za kitamaduni ni za kipepo. Baadhi kupitia marafiki, wengine kwa njia ya kusoma baadhi vipeperushi au riwaya. Mapepo yanakaa katika maeneo ya jirani na kila sanamu. Hufanya kazi kupitia sanamu katika mazoezi ya ibada ya sanamu (Zakaria 10 : 2). Kama sehemu ya dini, ibada ya sanamu inaweka chini nguvu ya Mungu na kuihamishia kwa viwakilishi vyake na kuvipa heshima ya Mungu vitu vilivoundwa (Warumi 1: 18-22). Maandiko yamefanua ibada ya sanamu kama uzinzi wa kiroho (Yeremia 3: 8-10). Hivyo mtoto wa Mungu unapaswa kuwa hauna uhusiano wowote , moja kwa moja au vinginevyo na ibada ya sanamu. Haya yanayoitwa maisha ya juu, juju na muziki ya disco huongozwa na Shetani na mapepo yake .

Mimi nakumbuka kwamba, kabla Bwana hajaniokoa, katika moja ya mikutano tuliyokuwa na Shetani, alisema: "Hii dunia ni yangu na mimi nitaenda kutawala dunia nzima katika uwezo wangu, nami nitawaharibu wote wanaoamini katika jina la mwenye haki. " Shetani hataji jina la Yesu. Kama mtu ye yeyote akifanya hivyo katika uwepo wake, basi anakuwa katika hatari ya kupoteza maisha yake. Aliahidi kutufanya sisi mawakala wake, magavana, nk Shetani ni mwongo na kwa kweli ni baba wa uongo. Pia kulikuwa na mipango ya kunyamazisha Wakristo Nigeria kwa kuzuia uingizaji wa Biblia na maandiko ya Kikristo.

Anafanya kazi kwa njia wasioamini katika nafasi ya uongozi na mamlaka ,ili kuanzisha sera na mipango ya kupambana na Kikristo. Anaanzisha vituo vya uponyaji ambavyo vitaonekana ni vya dini sana na kwa njia yao wanadai roho. Vituo hivi kawaida huitwa nyumba za kiroho za uponyaji ziko karibu nasi. Hapa maajabu mengi ya uongo yanafanyika kudanganya wateja wao. Shetani anafahamu mengi kuhusu ujio wa pili wa Yesu Kristo na mara kwa mara anataka mawakala wake kwa haraka kuwa katika utekelezaji wa shughuli zao, Huwa akisema: " Hatuna wakati uliobakia " Ndugu mtoto wa Mungu, Shetani halali , kwa nini wewe ulale ?

Sura8: Silaha ya Muamini

- JINA LA YESU
- DAMU YA YESU
- NENO LA MUNGU
- SIFA ZA KRISTO

« *Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.* » waefeso. 6: 9-10

« *Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao...* » Ufu. 12: 11

Nimekwisha sema mengi katika eneo hili, lakini kusema machache. Tambua kwamba kuna NGUVU katika Jina la Yesu! Kuna nguvu katika Damu ya Yesu! Maandiko yanasema: “ *Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba. Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.* (Philippians. 2: 8-11). Tena maandiko yanasema: “ *Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao* ” (Ufu. 12: 11). Acha jina la Yesu liwe katika midomo yako! Haya mawili,jina na damu, zinatawanya mipango ya shetani,na zaidi ni kwamba zinaharibu kabisa mipango ya shetani na mawakala wake.

Pili, lazima ujifunze kuimba nyimbo za sifa kwa Mungu daima. Kuna nguvu katika nyimbo za sifa. Kulikuwa na Mchungaji huyu - Mchungaji I.K. (jina limehifadhiwa). Alikuwa na kanisa Ebute Metta . Alikuwa ni tageti yangu na makosa yake yalikuwa :

1. Alikuwa anatusumbua kwa kufanya shughuli zake asubuhi na mapema i.e kuhubiri katika masaa ya mapema.
2. Alikuwa akitembea na kipaza sauti chake na anakiweka maeneo ya N.^o 2 Bus-stop sambamba na barabara ya Akintola, Ebute Metta. Alikuwa anahubiri. Hata acha pale kwenye kituo cha mabasi, ataendelea kukemea mapepo n.k.
3. Kanisani kwake atahubiri, ataweka wazi kazi za shetani, baada ya hapo ataendelea kufunga pepo.
4. Aliomba sana.
5. Alikuwa akiimba na kumsifu Mungu.

Nilituma wajumbe wangu naye lakini hawakuweza kumuua hivyo niliamua kutekeleza kazi hiyo mwenyewe. Siku hiyo, nilimuona akitembea kwenye njia ya G.R.A mpya. Kitu kizuri cha kutaja kuhusu Mchungaji huyu ni kwamba: Wakati wowote tuliotaka kumuende, tuliweza kuona nguzo ya wingu upande wake wa kuume na kushoto, vikitembea pamoja naye, hivi vilituzuia. Lakini siku fulani niliona hakuna kitu , hivyo nilikuwa na uhakika kazi yangu itafanikiwa sana. Nikaamuru mvua kunyesha ili niweze kumpiga kwa radi. Mvua ikaanza na radi ikaanza. Miti yote katika eneo ilianza kupoteza matawi yake, lakini Mchungaji huyu alikuwa akiimba nyimbo kwa furaha .Bado nakumbuka kiitikio : ” . **Katika Jina la Yesu kila goti litapigwa ”**

Kadiri alivyoendelea na kiitikio hiki mvua iliisha, radi ikatulia. Kukaonekana mara moja malaika wawili , mmoja kwa kila upande, na upanga wa moto. Macho yao na panga zao ni kama miale ya moto. Kisha upepo mkali

ukanikumba na nikajikuta katika mji mwingine! Kwa kweli nilichanganyikiwa, lakini kwa sababu tulikuwa wagumu, kile nilichokisema: "Mtu huyu ametoroka tena ! " Mchungaji hakujua vita vya kiroho ambavyo ilikuwa inapigana kwa niaba yake. Kwa hiyo, unaweza kuona, mtoto wa Mungu anavyolindwa. Biblia inaposema : "Hakuna kitu kwa njia yoyote kitawadhuru ninyi , " ina maana ya hicho inachokisema!

Ushahidi wa pili ni kuhusu Mkristo ambaye alipanda teksi pamoja nami. Alikuwa na wivu wa Mungu sana ndani yake na akaanza kusambaza vijitabu vya injili ndani ya teksi. Aliponipa kijitabu nilikataa. Akaanza kuhubiri. Hivyo nikawa nasumbuliwa nikaamua kumgonga kwa kidole changu chenye pete. Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kumuua. Kijana huyu akapiga kelele: " Damu ya Yesu! " Mara umeme na moto na malaika wakaonekana. Upepo mkali tena ukaliondoa kwa nguvu kubwa nje ya teksi mpaka katika msitu mnene. Kama ingekuwa si mtu ambaye naongozwa na nguvu za giza ningeweza kupotea katika msitu ule. Mkristo hakujua vita gani iliyopiganwa kwa niaba yake. Alichokijua pamoja na abiria wengine, ni kwamba nilitoweka kutoka kwenye teksi !

Jina la Yesu au Damu ya Yesu katika kinywa cha muumini kinatuma nje moto nk Maandiko yanasema: " *Jina la Bwana ni ngome imara; Mwenye haki huikimbilia, akawa salama.* " (Mithali 18: 10).

Ndugu msomaji, kama wewe ni mtoto wa Mungu , kumbuka kwamba Mungu ameliinua neno lake juu ya majina jina yake yote (Zaburi 138: 2), kwa hiyo kiri neno la Mungu (Neno la Mungu) na amini kwamba kile unasema kitakuja kupita, na itakuwa hivyo. **Hiyo ni ahadi ya Mungu !**

Tena ningependa kutaja hapa kwamba unaweza tu kukiri kile unachokijua. Kitabu kinatuamrisha sisi kukaa katika Neno la Mungu, kutafakari juu yake mchana na usiku. (Zaburi 01:02) Kwa wewe kuligawanya neno la kweli vyema,ni lazima kulijua. *Wakolosai 3:16 inasema: "Hebu neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote."* Tena Zaburi 1: 1-3 inasema: " Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenyewe mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa. "Kaa karibu na Biblia yako; Omba bila kukoma; na kuimba kwa moyo na kusimama, tumia mamlaka uliyopewa na Bwana Yesu Kristo!

Sura 9: Sasa nini kinafuata?

« Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure. »Ufu. 22: 17

Baada ya kusoma ushuhuda huu, hakuna haja ya mahubiri zaidi ili kutoa maisha yako kwa Yesu Kristo. Maandiko yanasema: " *Mwizi (Shetani) haji ila aibe , kuua na kuharibu. Mimi (Yesu Kristo) nimekuja mpate kuwa na uzima , na wawe nao tele* " (Yohana 10: 10).

Shetani anakuchukia na anapanga njia mbalimbali za kukuchukua kuzimu pamoja naye. Kwamba, unaweza kushuhudia kutokana ushuhuda huu. Ikiwa Shetani atatoa ahadi kwako na hata kukupa zawadi, unajua kwamba ina nia mbaya . Shetani ni mwongo na baba wa uongo. (Yohana 8:44) Mungu alimwita ni **adui yako**, kwa nini usimuamini Mungu na Neno lake?

Si kwa bahati mbaya kwamba umekutana na ushuhuda huu. Jichunguze na hakikisha uko katika Kristo. Ufanikiwa katika kujidanganya mwenyewe kama ukikuchagua kubaki kama ' **muenda kanisani tu** ' na mbaya zaidi ya yote , kama bado utaamua kuweka tabia ya Kutojishikamanisha kwa uamuzi huu muhimu zaidi katika maisha yako .

Sisi tunawasihi ninyi kwa niaba ya Kristo: **Mptanishwe na Mungu** . Kama wewe ni bado haujaokolewa, hii ina maana kulingana na Neno la Mungu haujamkubali Bwana Yesu Kristo kama Bwana wako na Mwokozi wako , kufuatia kwa njia ya ubatizo wa maji kwa kuzamishwa , tunakuhimiza kufanya hivyo bila kuchelewa.

Kesho inaweza kuwa umechelewa.

(Waebrania 3:15)

Ndugu aliyefasiri ufunuo huu ni Peter Kahale ni kijana aliyeokoka na anampenda Yesu na mwenye shauku ya kuhubiri injili ya Yesu Kristo.

Simu ya Mkononi: +255-769-610460, +255-653-610460.

Barua Pepe: kahalepeter@gmail.com.